# Nipashe

Ijumaa Mei 6, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580937

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



SportPesa

TZS. 1,224,601,040

BET LEO UWE BILIONEA

SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#




**Mbivu**, mbichi rufani hukumu ya Sabaya leo

UKURASA 4



GUARDIOLA: CITY TUNAHITAJI MUDA

UKURASA 21

# Wabunge wacharuka kupaa bei ya mafuta

UK. 2



"Lazima tupate watu watakaotuletea mafuta kwa bei nafuu, chochote kitakachotuhakikishia kutuletea bei nafuu tutakifanya."

**WAZIRI MAKAMBA**



"Iliwahi kushuka bei ya korosho, jeshi likaenda Mtwara hadi leo hakuna anayechezea bei ya korosho kwa sababu wanajua kitakachotokea."

**JOSEPH MUSUKUMA**



"Wabunge wana wajibu wa kusimamia na kuishauri serikali kwa kuwa wananchi wamewapa dhamana ya kuwasemea, kukaa kimya watakuwa hawawatendei haki wananchi."

**OMARY KIGUA**



"Soko la dunia ni Sh. 1,162 kwa lita moja, lakini tozo zilizopo kwenye mafuta zinafika Sh. 1,300, yaani tozo zinazidi bei ya mafuta."

**FESTO SANGA**








"Ninamwagiza Waziri Makamba siku ya Jumanne wiki ijayo aje na majibu ya namna ya kutatua jambo hili."

**SPIKA TULIA**



Hali hii ni kama UVIKO-19, tukakope mikopo ya bei nafuu, tuweke ruzuku kwenye mafuta."

**GRACE TENDEGA**

## Ajira 205,000 za makarani wa sensa zatangazwa

UKURASA 3

## Waziri Mkuu aanika upigaji na ufisadi ununuzi wa vifaa tiba

UK. 3


MICHEZO SIMBA, YANGA ZATAJA MWELEKEO UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA



Abiria wakiwa katika kituo cha daladala cha Kilombero, jijini Arusha jana, wakisubiri kumalizika kwa mgomo wa madereva waliotaka kuanza kutoza nauli mpya iliyotangazwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), kabla ya muda wake, ambapo mgomo huo, ulianza saa 11 alfajiri na kuisha saa nne asubuhi, baada ya Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Said Mtanda na viongozi wengine kuingilia kati. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wabunge wacharuka kupaa bei ya mafuta

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WABUNGE wameitaka serikali kuja na mkakati wa dharura wa kunusuru kupanda kwa bei ya mafuta, huku wengi wao wakitaka kupunguzwa kwa baadhi ya tozo kwenye mafuta pamoja na serikali kuomba mkopo wa dharura.

Mjadala huo uliibuka jana bungeni jijini hapo baada ya Mbunge wa Kilindi (CCM), Omary Kigua, kutoa hoja ya kutaka Bunge liahirishwe ili wabunge wajadili suala la kupanda kwa mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa.

Akitoa hoja hiyo, Kigua alisema kwa sasa kuna tatizo la kupanda kwa haraka kwa mafuta kulikosababisha kupanda kwa bei ya kila kitu kwa wananchi na nchi nzima kelele zimekuwa kubwa.

**WALICHOSEMA WABUNGE**

Mbunge wa Geita (CCM), Joseph Musukuma, alisema: "Tunaotoka vijijini mafuta tunauziwa Sh. 5,000 kwa lita moja. Hali ni mbaya sana. Iliwahi kushuka bei ya korosho, Jeshi likaenda Mtwara hadi leo hakuna anayechezea bei ya korosho kwa sababu wanajua kitakachotokea."

Alisema serikali inapaswa kuchukua hatua za dharura kuagiza mafuta ili kunusuru hali iliyopo sasa.

"Hili suala halikubaliki, kama kuna kodi tuliziweka kwenye mafuta tuziondoe kwa muda wa miezi mitatu. Pia tutenge kitu kwenye bajeti kunusuru. Nchi yetu inakopesheka, tukope ili tuokoe hili janga," alisema.

Mbunge wa Busega, Simon Lusengekile, alisema jambo la kupanda kwa bei ya mafuta ni hatari.

Alisema kuwa awali usafirishaji wa saruji kutoka Tanga hadi Mwanza kwa tani moja ilikuwa ni Sh. 130,000 lakini kwa sasa imefikia Sh. 160,000, kwamba hali hiyo inakwenda kupandisha bei ya mfuko wa saruji.

"Tufanye jambo la dharura, tupate fedha ya ruzuku kwenye mafuta. Mafuta yakishuka bei za bidhaa zitashuka. Pia tuangalie baadhi ya tozo tuzipunguze ili tulete unafuu kwa wananchi, bila mafuta maisha hayawezi kwenda, hivyo ni lazima tutafute fedha za dharura kunusuru jambo hili," alisema Lusengekile.

Mbunge wa Madaba, Joseph Mhagama, alisema kwa kipindi cha miezi miwili mafuta yamepanda kwa asilimia 92, akiwa na angalizo: "Mafuta ndiyo usalama wa maisha yetu, ndiyo ustawi wa taifa letu. Tozo zinazokwenda kujenga barabara, maji vijijini ziachwe lakini kuna zile ambazo hazina madhara nashauri zifutwe."

Mbunge wa Tarime Vijijini (CCM), Mwita Waitara, alisema: "Kuna mjadala mzito kwenye mitandao ya kijamii kuhusu kupanda kwa bei ya mafuta. Serikali ichukue hatua za haraka. Wenzetu Kenya wamekopa Sh. bilioni 850 kunusuru hali za wananchi. Serikali isikae vikao virefu, Watanzania wanaendelea kuumia."

Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Grace Tendega alisema: "Hali hii ni kama UVIKO-19, tukakope mikopo ya bei nafuu, tuweke ruzuku kwenye mafuta."

Mbunge wa Viti Maalum CCM, Neema Lukangira, alisema: "Serikali iondoe tozo za kitaasisi, kuitishwe mikutano ya dharura na taasisi za kimataifa zinazotudai ili watupunguzie namna ya kulipa madeni."

Mbunge wa Mlalo (CCM), Rashid Shangazi, alisema serikali ikakope Sh. bilioni 300 ili kunusuru hali iliyopo sasa, pamoja na kuweka ruzuku kwenye kila lita moja ya mafuta.

Mbunge wa Makete (CCM), Festo Sanga, alisema: "Hali ni mbaya. Makete wananunua mafuta Sh. 3,500 kwa lita. Bei ya mafuta katika soko la dunia ni Sh. 1,162 kwa lita moja, lakini tozo zilizopo kwenye mafuta zinafika Sh. 1,300, yaani tozo inazidi bei ya mafuta. Tutoe hizo tozo, tutafute pesa sehemu zingine tuweke kwenye mafuta."

**UFAFANUZI WA SERIKALI**

Akitoa ufafanuzi hoja hizo za wabunge, Waziri wa Nishati, January Makamba, alisema vita vya Ukraine na Russia ndivyo vilivyosababisha kwa asilimia kubwa kupanda kwa bei ya mafuta duniani.

Alisema asilimia 12 ya mafuta yote duniani yanazalishwa na Russia ambayo ni ya pili kwa uzalishaji baada ya Marekani.

"Ni hoja iliyokuja wakati mwafaka. Suala hili tumelichukua, serikali inawajali wananchi, imesikia kilio na inaungana nao katika kilio hiki na tumeanza kufanyia kazi.

"Lazima tupate watu watakaotuletea mafuta kwa bei nafuu, chochote kitakachotuhakikishia kutuletea bei nafuu tutakifanya," alisema.

Kuhusu hatua zilizoanza kuchukuliwa, Makamba alisema kwanza kunaandaliwa kuwapo kwa hifadhi ya mkakati wa mafuta na ndani ya wiki mbili zijazo kanuni zitakuwa zimeshakamilika.

Pili, alisema serikali inaandaa mfuko wa kuhimili bei za mafuta na andiko la kuanzisha mfuko huo linaendelea.

Waziri huyo aliitaja hatua ya tatu, serikali inaandaa kituo kikubwa cha biashara ya mafuta na ifikapo Mei mwaka huu, serikali itatia saini mkataba na sekta binafsi ili kuanzisha kituo hicho.

Hatua ya nne kwa mujibu wa Makamba, ni serikali inaandaa mkutano wa dharura na mawaziri wa nchi jirani utakaofanyika jijini Arusha kwa lengo la kujenga soko moja la mafuta la kikanda litakalosaidia kuwa na nguvu ya pamoja.

Aliitaja hatua ya tano ni serikali imefanya mazungumzo na mawaziri wa nishati wa nchi za Afrika zinazozalisha mafuta ikiwamo Algeria na Oman ili kupata unafuu wa kupata mafuta kwa bei nzuri.

**AGIZO LA SPIKA**

Baada ya mjadala huo, Spika Tulia alimwagiza Waziri Makamba kuwasilisha majibu bungeni wiki ijayo kuhusu mkakati wa muda mfupi wa serikali katika kukabiliana na dharura iliyojitokeza nchini.

"Nimewasikia wabunge kuhusu ushauri mlioutoa kwa serikali juu ya kupanda kwa bei ya mafuta. Hivyo, serikali itafanya nini katika jambo hili? Ninamwagiza Waziri Makamba siku ya Jumanne wiki ijayo aje na majibu ya namna ya kutatua jambo hili," aliagiza.

Dk. Tulia pia alisema mkakati wa muda mrefu wa serikali kuhakikisha bei ya mafuta haipandi utaelezwa bungeni siku zijazo.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
02.05.2022

TANGAZO

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **04.05.2022 hadi 17.05.2022** kampuni ya **Spedag Interfreight** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Holili kuelekea Moshi,** gari hilo lenye namba za usajili: **KDB189J / ZG5310 KCW052Z / ZG3212**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| Urefu | - | Mita 28.4 |
| Upana | - | Mita 5.0 |
| Kimo | - | Mita 5.6 |

3. Njia itakayotumika: **Holili hadi Moshi kupitia Soweto,** gari litasafiri muda wa mchana tu **( Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)**

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

216843002


## Bunge lataka hatua kukabili panya road

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

BUNGE limeliagiza Jeshi la Polisi kuhakikisha linaweka mbinu mbadala ili kutokomeza vitendo vya uhalifu mitaani vinavyofanywa na kundi la vijana, maarufu 'panya road'.

Limesema vitendo vinavyofanywa na kundi hilo havifanyiki jijini Dar es Salaam peke yake, bali vipo katika mikoa mbalimbali nchini, hivyo vinapaswa kukomeshwa.

Agizo hilo lilitolewa jana bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Vita Kawawa, alipowasilisha taarifa ya kamati hiyo pamoja na maoni yao kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Hivi karibuni vijana wanaotajwa kuwa ni 'panya road' walidaiwa kuwakata mapanga watu 19 na kupora mali Mtaa wa Mtongani Kata ya Kunduchi mkoani Dar es Salaam, huku Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam likithibitisha kuwakamata sita kati yao.

Kawawa alisema askari wa Jeshi la Polisi wanapaswa wasimamiwe inavyostahili ili kuzingatia sheria, taratibu, miiko, weledi na maadili ya Jeshi la Polisi katika utendaji kazi.

Alisema: "Dhana ya polisi jamii itekelezwe kwa ukamilifu katika kupambana na uhalifu hususani katika makazi ya watu, vitendo vya uhalifu vinavyofanywa na kundi linalojiita panya road vinapaswa kukomeshwa kwa Jeshi la Polisi kuja na mbinu mbadala."

Kawawa pia alisema ili kunusuru Taifa lisiendelee kupata hasara itokanayo na kuchakaa kwa hanga la kuhifadhi ndege za Jeshi la Polisi, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inapaswa kutoa kibali cha matumizi ya fedha za ukarabati na kuharakisha mchakato wa ununuzi.

Kuhusu Jeshi la Magereza, Kawawa alisema serikali inapaswa kusimamia maandalizi ya mpango mkakati wa muda mrefu wa unaotekelezeka wa kuwarejesha katika nchi zao wafungwa waliomaliza vifungo na bado wapo magerezani.

Pasipo kufanya hivyo, Kawawa alisema hali hiyo itaendelea kuchangia msongamano magerezani.

Kawawa alisema serikali pia inapaswa kuendelea kushughulikia tatizo la msongamano magerezani kwa kuweka utaratibu madhubuti wa kuiwezesha bodi ya Taifa na bodi za mikoa za Parole kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria.

Kuhusu Jeshi la Uhamiaji, Kawawa alisema serikali inapaswa iandae mpango mkakati unaotekelezeka wa kukabiliana na kumaliza wimbi la wahamiaji haramu kutoka nchi mbalimbali.

# Waziri Mkuu aanika upigaji na ufisadi ununuzi vifaa tiba

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa ameanika upigaji na ufisadi unaofanywa na wataalamu na watumishi wa umma katika ununuzi wa vifaa tiba huku akitaka hatua kali kuchukuliwa dhidi ya wahusika.

Pia ameiagiza Bodi ya Wataalamu ya Ununuzi na Ugavi (PSPTB) kuwachukulia hatua haraka waliohusika na upotevu wa fedha za UVIKO -19 zilizotolewa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya afya kwenye hospitali za rufani, wilaya, zahanati na vituo vya afya.

Sambamba na hilo, amehimiza hatua hizo zichukuliwe haraka kabla ya yeye kutembelea Jumatatu Bohari Kuu ya Dawa (MSD) akiambatana na Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kupata maelezo ya kina juu ya wizi huo.

Akizungumza jana jijini Arusha wakati akizindua Wiki ya Ununuzi wa Umma, Majaliwa alisema kitendo kilichofanywa na wasimamizi wa ununuzi wa umma ambao wanaaminiwa na serikali, hakivumiliki.

Akitoa mfano wa MSD ambayo ilitakiwa kununua kipimo cha sukari ambacho kwa bei ya kawaida ni Sh. 150 lakini ikanunua kwa Sh. 300 huku kipimo cha mkojo bei ikiwa Sh. 200 ikanunua kwa Sh. 780. Pia ilinunua kipimo kidogo cha hamolojia ya mwili kwa Sh. 4,500 wakati bei halisi ni Sh. 2,100. "Lakini pia walipaswa kununua kipimo kikubwa cha haimolojia ya mwili bei ya kawaida ni Sh. 3,800 wao wamenunua kwa Sh. 6,300. Si mnaona hizi bei zinavyokwenda? Watu hawana huruma na Watanzania wenzao," alisema.

Majaliwa aliendelea kutoa mfano wa upigaji huo kuwa kipimo cha kuangalia ufanyaji kazi wa figo ambacho ni muhimu sana na vingepatikana kwa wingi kinachouzwa Sh. 6,000 lakini kimenunuliwa kwa Sh 40,000. Pia alisema MSD ilitakiwa kununua mashine ndogo ya kipimo cha haimolojia ya mwili ambacho kinauzwa Sh. milioni tano lakini ikanunua kwa Sh. milioni 14.045 na mashine ndogo ya kupima kemia ya mwili ambayo bei ya kawaida ni Sh. milioni 1.35 imenunuliwa kwa Sh. milioni 6.7.

"Hawa walitakiwa kununua mashine kubwa ya kupimia haimolojia ya mwili. Hiki kifaa kinauzwa Sh. milioni 20.8 lakini wamenunua Sh milioni 117. Hawa pia walitakiwa wanunue mashine ya kupimia haimolojia ya mwili cha ukubwa kidogo bei ya kawaida ni Sh. milioni 37.4 wao wamenunua Sh. milioni 149.4.

"Hebu wataalamu wetu mtuambie ni kwa sababu ya nini? Wataalamu wetu wa manunuzi (ununuzi) kwa nini hili linatokea na kwa maslahi ya nani? Je, tukichukua hatua tena kali, vyombo vyote mko hapa vya ununuzi, haya ndiyo yanayoendelea kwenye ofisi zetu kwa wale wachache wasiokuwa na nia njema na fedha za walipakodi wa nchi hii," alisema.

Alisema kuwa ongezeko hilo la fedha zilizopotea kwa ujanja wa watu wasiozingatia sheria, taratibu, kanuni za ununuzi wa umma zingenunua vifaa kwa wingi, lakini wamenunua kifaa kimoja tu huku Watanzania wakisubiri kupata vifaa vingi visambae kwenye hospitali, zahanati na vituo vya afya.

# Ajira 205,000 makarani sensa zatangazwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imetangaza ajira 205,000 za makarani na wasimamizi wa Sensa ya Watu na Makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti 23, mwaka huu huku ikisisitiza hakutakuwa na maombi yatakayofanyiwa kazi zaidi ya yale yatakayofuata utaratibu uliowekwa mtandaoni.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera na Uratibu wa Bunge, George Simbachawene, alibainisha hayo jana alipokuwa akitoa taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu kuanza mchakato wa ajira za makarani na wasimamizi wa sensa.

"Kwa niaba ya mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Kamati ya Taifa ya Sensa, napenda kutangazia Watanzania wenye sifa na wenye kuhitaji kuomba nafasi hizi kwamba mchakato wa kuwapata makarani na wasimamizi wa sensa utaanza leo (jana) tarehe 5 hadi tarehe 19 Mei, 2022.

"Nipende kuweka wazi kwamba ajira hizi zitaombwa kupitia mtandao (Online) na hazitahusisha malipo ya aina yoyote kwa mwombaji wa ajira," alisisitiza Simbachawene. Alisema mchakato wa kuchambua maombi ya kazi pamoja na usaili utasimamiwa na kamati maalum itakayoundwa katika ngazi ya kila wilaya na usaili utafanyika katika ngazi ya kata kwa nafasi za makarani na wasimamizi wa maudhui katika ngazi ya wilaya kwa wasimamizi wa TEHAMA.

"Niwaombe Watanzania wote wenye sifa ambao wangependa kuomba nafasi za ajira za makarani na wasimamizi wa sensa kufuata utaratibu uliowekwa kwa ukamilifu ili kuomba nafasi hizo," alisema.

Kadhalika, alisema kazi za kufanya pamoja na sifa za mwombaji zimebainishwa katika tangazo la ajira za muda za makarani na wasimamizi wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022.

"Hakutakuwa na maombi yatakayofanyiwa kazi zaidi ya yale yatakayofuata utaratibu uliowekwa mtandaoni.

"Kumekuwapo na watu au makundi ya watu wenye nia isiyo njema kwa zoezi la sensa ambao wamekuwa wakijaribu kutoa matangazo ya ajira hizo kwa nia ya kuwatapeli wananchi wanaohitaji kushiriki katika zoezi hili na pengine kwa nia ya kuvuruga mchakato mzima serikali itaendelea kuwafuatilia na kuwachukulia hatua kali watu wote wenye nia ovu ya kuharibu zoezi hili," alisema. Pia, alisema kutokana na hali hiyo serikali imetangaza rasmi kuanza kwa mchakato wa ajira za makarani na wasimamizi kuanzia jana hadi Mei 19, mwaka huu, ambao utahusisha wasimamizi wenye sifa stahiki na watakaofanya kazi katika maeneo yao wanayoishi.

Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi mwaka 2022 na Spika mstaafu wa Bunge, Anne Mkinda alisema maandalizi ya zoezi hilo yamekamilika kwa asilimia zaidi ya 81.

"Maandalizi kwa ujumla yamekamilika kwa takribani zaidi ya asilimia 81 na hivi sasa tumetangaza ajira hizi za makarani na wasimamizi wa sensa ya watu na makazi hivyo wito wangu kwa Watanzania wenye sifa kujitokeza kuomba kwani tukipata makarani wasio na sifa zoezi zima litaharibika," alisema Makinda.

CRDB BANK
*Tunakusikiliza*

## Mkutano Mkuu wa Ishirini na Saba wa Wanahisa

*Mwenyekiti na Wanahisa,*

**Yah: Taarifa ya Mkutano Mkuu wa Ishirini na Saba**
Taarifa inatolewa kwamba **Mkutano Mkuu wa Ishirini na Saba** wa CRDB Bank Plc utafanyika siku ya Jumamosi tarehe **21 Mei 2022**, katika **Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC)**, Ukumbi wa Simba na kwa njia ya kidijitali kuanzia saa tatu kamili **(Saa 3.00) asubuhi** kujadili dondoo zifuatazo:

1. **Kufungua Mkutano.**
2. **Kuridhia Dondoo.**
3. **Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Ishirini na Sita.**
4. **Kujadili yatokanayo na kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Ishirini na Sita.**
5. **Kujadili na kupokea Ripoti ya Wakurugenzi wenye dhamana ya Uongozi na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za mwaka 2021.**
   5.1 Ripoti ya Wakurugenzi wenye dhamana ya Uongozi.
   5.2 Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2021.
   5.3 Gawio kwa mwaka 2021.
6. **Kuidhinisha ada ya Wakurugenzi.**
7. **Kuteua Wakaguzi wa Hesabu.**
8. **Kuchagua Wajumbe wa Bodi**
   8.1 Wajumbe watatu (3) wa Bodi watakaowakilisha kundi la wanahisa wenye hisa chini ya asilimia moja (1%).
   8.2 Mjumbe mmoja (1) wa Bodi atakayewakilisha kundi la wanahisa wenye hisa kati ya asilimia moja na kumi (1% na 10%).
   8.3 Mjumbe mmoja (1) Huru wa Bodi
9. **Kujadili mapendekezo kutoka kwa Wanahisa.**
10. **Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti.**
11. **Kupanga mahali na tarehe ya Mkutano ujao.**
12. **Kufunga Mkutano.**

***MAELEZO***
1. **Mahudhurio kwa njia ya Kidijitali***: Mwanahisa anaweza kuhudhuria Mkutano Mkuu kwa njia mbalimbali za kidijitali (SIM Banking, SIM Account na tovuti [https://www.crdbbank.co.tz]). Benki itawatumia wanahisa wote kupitia simu zao za mkononi utambulisho na maelekezo kuhusu jinsi ya kujiunga na kushiriki Mkutano Mkuu kidijitali.*
2. *Daftari la Wanahisa litafungwa tarehe 13/05/2022 na litafunguliwa tena tarehe 16/05/2022.*
3. *Mapendekezo kutoka kwa wanahisa yatakayojadiliwa katika dondoo namba 9 yatumwe na yamfikie Katibu kabla ya **Ijumaa tarehe 06/05/2022 saa 10.00 jioni.***
4. *Makabrasha ya Mkutano Mkuu yatapatikana matawini na yanaweza kuchukuliwa kuanzia tarehe **10/05/2022**, yatapatikana pia Arusha kwenye ukumbi wa Mkutano tarehe **20 hadi 21 Mei 2022**. Pia makabrasha ya Mkutano Mkuu yatapatikana kwenye tovuti ya benki kuanzia tarehe 10/05/2022.*
5. *Wanahisa wanaotaka kuhudhuria Mkutano Mkuu watajigharamia usafiri na malazi.*

**TAARIFA YA SEMINA KWA WANAHISA**
Taarifa inatolewa kwamba kutakuwa na Semina kwa Wanahisa itakayolenga kutoa elimu kuhusu Umuhimu na taratibu za kuandaa Wosia na Mirathi, Kusitisha utoaji wa Risiti za Uwekezaji na Umuhimu wa kulinda Mali zako itafanyika Ijumaa, tarehe 20/05/2022 katika **Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC), Ukumbi wa Simba** kuanzia saa **3.00 asubuhi**.

Kwa mawasiliano tumia anuani ifuatavyo:
**Katibu**
**CRDB Bank Plc**
**CRDB Bank Head Quaters**
**S. L. P. 268**
**Dar-es-Salaam**
**Simu. na. 022 - 2114237, 2117442 - 7 - Fax na. 022 - 2131005**
**Barua pepe –shares_unit@crdbbank.co.tz**

**KWA IDHINI YA BODI**

J. B. Rugambo
**KATIBU**

20 Aprili, 2022

216841202

# Mbivu, mbichi hukumu rufani ya Sabaya

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Arusha, leo inatarajia kutoa hukumu ya rufani namba 129, katika kesi ya jinai iliyokuwa inamkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya na wenzake wa wawili.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Silvester Nyegu na Daniel Mbura, waliokuwa wakikabiliwa na mashtaka matatu ya unyang'anyi kwa kutumia silaha.

Februari 14, mwaka huu, mahakama hiyo ilianza kusikiliza hoja 14 za waleta rufani kupinga adhabu ya hukumu ya kifungo cha miaka 30 kwenda jela iliyotolewa na Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mkoa wa Arusha.

Oktoba 15, mwaka 2021, Hakimu Mwandamizi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha, Odira Amworo, alimtia hatiani Ole Sabaya na wenzake kuhukumiwa kifungo cha miaka 30 jela.

Katika rufani hiyo, mawakili wa wapeleka rufani katika kesi hiyo, walikuwa ni Mosses Mahuna, Fauzia Mustafa, Majura Magafu, Edmund Ngemela, Silvester Kahunduka na Fridolin Bwemelo.

Kadhalika, katika kesi hiyo, mawakili wa wajibu rufani ni Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ofmedy Mtenga, Wakili wa Serikali, Baraka Mgaya na Wakili wa Serikali, Veridia Mlenza, na rufani ilisikilizwa chini ya Jaji wa mahakama hiyo, Sedekia Kisanya, kutoka Mahakama Kuu, Kanda ya Musoma.

Wakati akitoa hukumu hiyo, hakimu Amworo, alisema kutokana na ushahidi uliotolewa mahakamani huko, mahakama imewatia hatiani na kuwahukumu miaka 30 kwenda jela kwa kutenda makosa matatu.

Alisema kosa la kwanza na la pili ni la unyang'anyi wa makundi pasipo kutumia silaha, na kosa hilo lilifanywa na washtakiwa wote kwa pamoja kwa kuwa waliwatendea Numan Yasin na Ramadhani Rashid (mashahidi wa Jamhuri), katika duka la Mohamed Saad, lililoko Mtaa wa Bondeni, jijini Arusha.

Kosa la tatu alisema ni la unyang'anyi wa kutumia silaha ambalo washtakiwa hao, walimtendea Bakari Msangi, kwa kumpiga, kumfunga pingu, kumtishia silaha na kumpora fedha Sh. 390,000.

Hakimu alisema hakuna ubishi kwamba Sabaya akiwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, alitenda makosa hayo kinyume na sheria.

Pia, alisema kwa kuwa mikono yake imefungwa na sheria hawezi kutoa adhabu ya zaidi ya kifungo cha miaka 30 japokuwa washtakiwa hatiani kwa makosa matatu ambayo kila kosa kifungo chake ni miaka 30 na watatumikia adhabu hiyo kwa pamoja.

Alisema kosa la kwanza, la pili na la tatu ni kifungo cha miaka 30 kwa kila kosa na wakati mwingine kifungo kinakwenda sambamba na adhabu ya viboko hivyo alikataa ombi la wakili wa Jamhuri kifungo kwenda sambamba na viboko.

Sabaya na wenzake walikuwa wanakabiliwa na mashtaka matatu likiwamo la kwanza la unyang'anyi wa kutumia silaha.

Ilidaiwa mahakamani huko Februari 9, mwaka 2021, wakiwa Mtaa wa Bondeni, Jiji la Arusha, katika duka la Sahiid Store, wote kwa pamoja wakiwa na silaha walifanikiwa kumpora Bakari Msangi, Sh. 390,000 na simu mbili na kabla ya uporaji walimshambulia kwa kumpiga ngumi, mateke, kofi na kumtishia kwa silaha.

Shtaka la pili lilikuwa linawakabili wote kwa pamoja na ilidaiwa kwamba Februali 9, mwaka 2021, walipora fedha kaunta katika duka la Mohamed Al Saad, Sh. 2,769,000 na kabla ya uporaji waliwapiga mateke, makofi na kuwatisha kwa silaha watu waliokuwapo na kuchukua kiasi hicho cha fedha.

Shtaka la tatu unyang'anyi wa kutumia silaha lilikuwa likiwakabili washtakiwa wote.

Ilidaiwa mahakamani huko, Februari 9, mwaka 2021, katika Mtaa wa Bondeni, jijini Arusha wakiwa na silaha walipora simu moja ya mkononi, Sh. 35,000 mali ya Ramadhani Rashid na kabla ya kufanya uhalifu huo waliwaweka chini ya ulinzi watu wote waliokuwa ndani ya duka la Mohamed Saad.




Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kaskazini, Dismas Prosper (wa pili kushoto), akikabidhi fulana zilizotolewa na benki hiyo, kwa Ofisa Ugavi wa Wizara ya Fedha na Mipango, Hilda Segere, kwa ajili ya wiki ya manunuzi ya umma iliyoanza jijini Arusha jana. Kushoto ni Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Clocktower, Emmanuel Kishosha na Ofisa Habari wa Wizara hiyo, Saidina Msangi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yawaita wawekezaji wa Norway na Uingereza

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amewaalika wafanyabiashara na wawekezaji kutoka nchi za Norway na Uingereza kuja kuwekeza katika sekta mbalimbali za uchumi na huduma Tanzania hususani kwenye sekta ya ujenzi wa miundombinu.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufungua mkutano uliowaleta pamoja watendaji wa taasisi za serikali na ujumbe wa wawekezaji na wafanyabiashara 37 kutoka Norway na Uingereza ulioratibiwa na Norwegian-African Business Association na Kampuni ya Invest Africa kwa kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC), Prof. Mbarawa aliwahakikishia wawekezaji hao kuwepo kwa mazingira mazuri ya uwekezaji na kufanya biashara.

Amesema uwekezaji katika sekta ya miundombinu hususani ujenzi wa barabara na reli itasaidia kufungua fursa lukuki za kibiashara na uwekezaji kwenye nyanja zingine za kiuchumi na kijamii zilizoko hapa nchini.

"Mpaka hivi sasa kwa upande wa mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa wa SGR umefikia asilimia 97, lakini hii inatoa haitoshi kwa kuwa kuna baadhi ya maeneo nchini bado yanahitaji huduma ya reli kwa kuwa ni maeneo yenye shughuli kubwa za uzalishaji," alisema Prof. Mbarawa.

Prof. Mbarawa aliongeza kuwa suala la uboreshaji wa miundombinu haiitaji nguvu ya serikali pekee kwa kuwa serikali inatoa fursa kwa wadau na wawekezaji kuwekeza nchini jambo ambalo limekuwa likifanywa hata na mataifa yaliyoendelea.

"Ninachukua nafasi hii kuwahamasisha muje kwa wingi na serikali yetu sikivu iliyo chini ya Rais Samia Suluhu Hassan inawathamini wawekezaji hasa kwenye kuwashirikisha kwenye miradi mikubwa ya miundombinu ambayo itakwenda kuifungua nchi kimaendeleo na kutoa fursa kubwa ya ajira nchini," lisema Prof. Mbarawa.

Mkurugenzi Mtendaji TIC, Dk. Maduhu Kazi, mbali ya kuwahakikishia ushirikiano mkubwa wafanyabiashara na wawekezaji hao, alibainisha kuwa kituo hicho kitaendelea kutengeneza mazingira mazuri ili kuvutia zaidi na kurahisisha shughuli za uwekezaji nchini.

"Ninapenda kuchukua fursa hii kuwakaribisha sana kuwekeza nchini hasa kwenye maeneo ya fedha, uvuvi, usafirishaji, kilimo na uchukuzi, na niwatoe wasiwasi kwa kuwa serikali imeweka mazingira mazuri zaidi ya uwekezaji," alisema Dk. Maduhu.

Dk. Maduhu aliongeza kuwa: "Serikali inamatarajio makubwa na nyinyi kuja kuwekeza nchini na hii inadhihirisha kwa kuwa Rais wetu amekuwa mstari wa mbele kuhamasisha uwekezaji na kuitangaza nchini jambo ambalo limepokelewa vizuri na wawekezaji."

# TPA: Tunazingatia usalama, afya kazini

**Na Mwandishi Wetu**

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imesema inazingatia kikamilifu matumizi ya vifaa kinga na tahadhari muhimu za kulinda afya za watumishi katika sehemu za kazi ili kuhakikisha rasilimali hiyo muhimu katika Mamlaka hiyo inakuwa salama wakati wote.

Kauli hiyo ilitolewa na Kaimu Mkurugenzi wa Masoko na Uhusiano wa TPA, Nicodemus Mushi, wakati wa maonyesho ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi yaliyoandaliwa na Osha jijini Dodoma.

Alisema mazingira ya kazi ya TPA yanahusisha shughuli katika maji wakati wa kuhudumia meli, matumizi ya mashine na mitambo mikubwa katika kupakia, kupakua shehena na katika hatua mbalimbali za ujenzi wa miundombinu.

Alisema mazingira haya yanaweza kusababisha madhara kwa Watumiaji pale kunapokosekana umakini au zinapopata hitilafu za kiufundi.

Kwa kutambua hilo, kitengo chetu za zimamoto na usalama kinafanya juhudi kubwa ya kutoa elimu na kusimamia kikamilifu uzingatiwaji wa hatua zote za tahadhari na matumizi sahihi ya vifaa kinga wakati wote wa utekelezaji wa majukumu bandarini," alisema.

Mkurugenzi wa Huduma za Meli na shughuli za Kibandari wa TPA, Abdallah Mwingamno, alisema maonesho hayo yana umuhimu mkubwa kwa kuwezesha umma kukutana na taasisi mbalimbali na kupata elimu na kujionea vifaa mbalimbali vinavyotumika kulinda afya za watumishi wawapo kazini.

"TPA inathamini sana usalama wa watumishi wake, wateja na wadau wanaofanya kazi zao katika maeneo ya bandari ili kuwahakikishia usalama wa afya zao na mali zao katika maeneo yote ya bandari. Tunasimamia kikamilifu matumizi ya vifaa kinga, tunatoa matangazo katika maeneo mbalimbali ya bandari ili kuwakumbusha wadau jinsi ya kuwa salama wawapo bandarini," alisema na kuendelea:

Tunaishukuru menejimenti kwa kuendelea kuwekeza katika mafunzo, elimu na upatikanaji wa uhakika wa vifaa kinga na vitendea kazi mbalimbali vya kujikinga dhidi ya ajali na majanga yanayoweza kujitokeza Bandarini kama vile ajali za mashine, mitambo, magari na hata moto."

# Waziri ayataja makundi matatu msamaha WCF

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, ameyataja makundi matatu yatakayonufaika na msamaha wa riba kwa waajiri waliochelewa kuwasilisha michango katika Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF).

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam katika ofisi za WCF zilizoko Victoria, Prof. Ndalichako alilitaja kundi la kwanza ni waajiri waliokwishalipa malimbikizo ya michango wanayodaiwa na mfuko na wamebakiza deni la riba peke yake.

Alilitaja kundi la pili ni la waajiri wote watakaolipa malimbikizo ya michango ya miezi ya nyuma wanaodaiwa na mfuko kabla ya Juni 30, mwaka huu kuwa watanufaika na msamaha wa ondoleo la riba ya michango kwa miezi tajwa.

"Kundi la tatu ni waajiri wote ambao sasa hawajajisajili kwenye Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi watakapojisajili na kulipa michango stahiki inayodaiwa kabla ya Juni 30, mwaka huu," alisema.

Prof. Ndalichako alisema hadi kufikia Agosti 2021 takribani waajiri 13,468 wa sekta binafsi na waajiri 191 wa sekta ya umma walikuwa kwenye orodha ya madeni ya riba

"Kwa mamlaka niliyopewa chini ya kifungu 75 (5) cha Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi Sura 263, ninatangaza msamaha wa riba iliyotozwa kwa kipindi cha kuanzia Oktoba Mosi mwaka 2017 hadi Agosti 31, mwaka 2021 kwa waajiri wote waliochelewa kuwasilisha michango katika mfuko huu wa WCF kwa kipindi hicho," alisema.

Waziri huyo aliwataka waajiri kutumia vizuri msamaha huo uliotolewa na serikali unaolenga kuongeza kiwango cha utekelezaji wa hiari wa sheria ya fidia katika kuhakikisha wanajisajili kwenye mfuko na kulipa malimbikizo ya nyuma bila kutozwa riba.

Alisema michango inayotolewa na waajiri hutumika kulipa wafanyakazi fidia pale mfanyakazi atakapopata ajali ama ugonjwa kutokana na kazi na iwapo bahati mbaya atafariki, italipwa kwa wategemezi wake.

"Tangu Julai 2015 hadi kufikia Agosti 2021, michango iliyocheleweshwa ilikuwa ikitozwa riba ya asilimia 10 kwa mwezi. Hata hivyo, serikali iliamua kushusha kiwango cha riba kutoka asilimia 10 hadi asilimia mbili kwa mwezi kuanzia mwezi Septemba mwaka 2021, ili kutoa nafuu kwa waajiri na kuweka mazingira rafiki ya biashara na uwekezaji nchini," alifafanua.

Prof. Ndalichako alisema michango itakayolipwa baada ya kipindi kilichowekwa kisheria itatozwa riba.

Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dk. John Mduma, aliishukuru serikali kukubali kutoa punguzo hilo kwani linarahisisha usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya mfuko. "Tunaishukuru serikali na tunaamini msamaha huu utasaidia utekelezaji wa majukumu yetu pia kuhamasisha waajiri kuitikia kwa hiari," alisema.

# Mwinyi apongeza WFP kusaidia maendeleo

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amepongeza mikakati na mipango iliyowekwa na Shirika la Chakula Duniani (WFP), kwa ajili ya kusaidia maendeleo ya Zanzibar.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana alipofanya mazungumzo na Mwakilishi Mkaazi wa WFP Tanzania, Sarah Gordon-Gibson.

Alipongeza hatua za WFP kuongeza mikakati na mipango ya kuhakikisha Zanzibar inafaidika moja kwa moja na huduma inazozitoa katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo.

Rais Mwinyi alifurahishwa na dhamira ya shirika hilo kushirikiana na serikali katika kukabiliana na maafa, uwezeshaji kiuchumi kwa wanawake hasa wakulima wa mwani, lishe na usalama wa chakula, kuwasaidia wakulima wadogo katika ujenzi wa barabara za ndani na kuwasaidia katika mnyororo wa usafirishaji wa bidhaa.

Pia Dk. Mwinyi alizipongeza juhudi zilizoanza kuchukuliwa na shirika hilo kuanza mazungumzo na baadhi ya sekta husika katika kuendeleza programu hizo.

Rais Dk. Mwinyi alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kutoa ushirikiano kwa WFP katika kuhakikisha linatekeleza vyema shughuli zake Zanzibar.

Aidha, alipongeza maeneo ambayo shirika hilo limekusudia kuongeza nguvu zake ikiwa ni pamoja na kuwasaidia kinamama wanaolima zao la mwani kwa kuwaongezea uwezo kwa kulipata thamani zao hilo pamoja na kuwatafutia soko la uhakika.

Dk. Mwinyi pia aliipongeza azma ya WFP ya kurejesha huduma ya chakula kwa watoto shuleni hatua ambayo itawaongezea ufahamu sambamba na kuwasaidia watoto kuwa na lishe bora.

Alisema shirika hilo limekuwa likifanya kazi vyema nchini na azma yake ya kuongeza mikakati yake katika programu ilizojiwekea itasaidia jamii kwa kiasi kikubwa wakiwamo wanawake na watoto.

Naye Gordon-Gibson alimweleza Rais Mwinyi mikakati na mipango iliyowekwa na WFP kwa Zanzibar katika kipindi cha miaka mitano kuanzia Julai, mwaka huu hadi 2027 itaongezwa.

Alisema WFP imeshapanga programu kadhaa ambazo Zanzibar itafaidika kwa kiasi kikubwa katika kipindi cha miaka mitano zikiwamo kuwawezesha wanawake hasa wakulima wa mwani, kukabiliana na maafa, lishe na usalama wa chakula, kuwasaidia wakulima wadogo.

Gordon- Gibson alieleza jinsi shirika hilo linavyofanya kazi zake za kutoa huduma zikiwamo za chakula kwa wakimbizi kwa kule Tanzania Bara pamoja na nchi nyengine za jirani.

Mwakilishi huyo alipongeza ushirikiano mzuri anaoupata kupitia shirika hilo hapa Zanzibar na kuahidi kuendelea kutoa ushirikiano wake ili Zanzibar izidi kupata mafanikio katika sekta zake za maendeleo.


**TUMAINI SAVINGS AND CREDIT COOPERATIVE SOCIETY LIMITED (TUMAINI SACCOS LTD)**

**JOB OPPORTUNITY**

Tumaini SACCOS is a member based financial Institution registered under the Cooperative Society Act, with the main objective of mobilizing savings and advancing loans to members in accordance with the SACCOS Loan policy.

Tumaini SACCOS based in Arusha is seeking to recruit suitably qualified candidate for the following vacant position.

**TITLE: SENIOR ACCOUNTANT**

**REPORTS: SACCOS MANAGER**

**General Responsibility:**

AdviceSACCOS Manager on finance issues, Managing SACCOS fund, Put fund and risk control measures. Manage and supervise accounts teamin regard to day to day activities; to ensure adequate and smooth financial operations.

**Duties and Responsibilities**

1. Prepare monthly, quarterly, and annual financial reports and provide income and expenditure reports both for internal and external use,
2. Supervise the proper maintenance of Tumaini SACCOS' books of accounts.
3. Prepareannual budgets, and annual financial projections.
4. Ensure adherence to all financial policies and procedures.
5. Advise SACCOS Manager in making investment decisions.
6. Monitor Cash flow movement register.
7. Maintain subsidiary ledger accounts including staff advances
8. Supervise and mentor the Accountant.
9. Facilitate both Audit exercise and inspections; following up Audit & Inspections recommendations.
10. Provide guidelines to operational staff in areas of loan portfolio management.
11. Provide guidelines to statutory compliance issues including tax issues, monthly BOT/TCDC reports and other statutory obligation (NSSF, WCF, SDL, HELSB and PAYE).
12. In charge the SACCOS motor vehicles.
13. Carry out any other duties as may be assigned by the Board of Directors or SACCOS Manager.

**Knowledge, Skills and Abilities Required**

- A holder of Degree or Advance Diploma in Accountancy from a recognized institution, and CPAHolder.
- Masters Degree in Finance, Accounting, Business Administration, Taxation and SACCOS Management will be an added advantage.
- Ability to work with only minimal supervision.
- Ability and desire to learn new things.
- Experience with computer packages including Microsoft Office, and financial databases.
- Ability to communicate fluently in speaking, reading and writing in Kiswahili and English.

**Experience**

Minimum 3 years' experience in a reputable organization.

All interested candidates are required to address their application letters and CVs to;

**Chairperson,**
**Tumaini SACCOS Limited,**
**Box 6070,**
**Arusha.**

All applications should me sent to email address: johnson_robinson@wvi.org

Applications should be received not letter than **27May 2022, official hours.**




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Elimu kuhusu rushwa ianzie ngazi ya msingi

**RUSHWA** imekuwa ikileta vilio karibu sekta zote ikiwamo ya elimu, sehemu ya kazi na maeneo mengine ya kutolea huduma za kijamii, na kukwamisha shughuli za maendeleo kwa mtu mmoja au kwa jamii.

Kuwapo kwa rushwa kuna chimbuko lake ambalo ni mmomonyoko wa maadili ambao huanzia katika ngazi ya familia hadi taifa, hivyo vita dhidi yake si ya serikali tu, bali kukuza maadili kunahitaji wadau wote na jamii kwa ujumla wake.

Tunasema hivyo kwani mmomonyoko huo ndio unaozaa maovu ikiwamo tatizo la rushwa ambalo sasa ni sugu katika maeneo mbalimbali kuanzia shuleni, sehemu za kazi na kwingine.

Kutokana na hali hiyo tunashauri wazazi, walezi na jamii kushiriki kikamilifu katika malezi bora yatakayosaidia watoto kuwa raia wema kuanzia nyumbani, shuleni ili hata wakiwa watu wazima, waendelee na kusimama katika maadili mema.

Pamoja na hilo, tunashauri pia kuwapo kwa mitaala kwa ajili ya somo la maadili, ambalo litakasaidia wanafunzi kuitambua rushwa na madhara yake wangali wadogo, kwani chanzo cha rushwa ni mmomonyoko wa maadili. Tunaunga mkono juhudi mbalimbali ambazo zimekuwa zikifanywa za kupambana na rushwa zikiwamo za kuanzisha klabu za wapinga rushwa shuleni ili wanafunzi wapate elimu ya madhara ya tatizo hilo. Hatua hiyo ni nzuri kwa sababu inawaandaa wanafunzi kupinga rushwa wangali wadogo hata pale wanapokuwa watu wazima waendelee kupambana nayo kwa manufaa yao na ya taifa kwa ujumla.

Kwa mfano, wanafunzi wanatakiwa kujua rushwa ni nini, ikiwamo ya ngono, fedha na vitu vingine badala ya kuisikia tu bila kujua maana yake na madhara yake na kujikuta wakijiingiza humo.

Hivyo tunadhani sasa ni wakati mwafaka wa kuwapo kwa mikakati ya kuhakikisha wanafunzi kuanzisha shule za msingi hadi juu wanapata elimu kuhusu rushwa.

Siyo vibaya kuiga kile ambacho kinataka kutekelezwa katika Shule ya Sekondari Kibiti mkoani Pwani kwa kuanzisha midahalo ya wazi kuelimisha kuhusiana na mapambano ya rushwa kwa wanafunzi wa shule hiyo.

Tunaamini viongozi na watumishi bora wa umma, huandaliwa tangu mwanzo, kwa hiyo suala la kuanzisha somo la maadili shuleni ni la muhimu ili kuchangia kuandaa viongozi watakaoleta mapinduzi chanya ya kiuchumi kwa nchi yetu.\

Wanafunzi wakipata elimu kuhusu rushwa na madhara yake, tunaamini ni kuwa hata watakapokuwa wakubwa wataendelea kuichukia, kutokana na ukweli kwamba inakwamisha maendeleo na inaua uchumi.

Serikali imekuwa ikisisitiza kuwa utawala bora ni kipaumbele cha kufikia Malengo ya Maendeleo ya Taifa, kwamba utawala bora umekuwa ni jambo muhimu katika kukuza, kuimarisha amani na mengine mengi.

Tunashauri Mkakati wa Taifa wa Dhidi ya Rushwa wa mwaka 2017-2022 ambapo awamu ya tatu ya mkakati huo ni mwendelezo wa juhudi za serikali za kuunga mkono mapambano dhidi ya rushwa.

Utaratibu wa utoaji wa elimu kuhusu rushwa kutolewa kuanzisha shule za msingi tunauona kama mtazamo mpya unaolenga kuhakikisha rushwa inaondolewa nchini kuanzia sasa na hata baadaye.


Kwa upande mwingine elimu kuhusu rushwa kuanzia ngazi ya shuleni ni uamuzi sahihi kwa kuwa watoto wakipata uelewa mapema kuhusu athari zake, itasaidia kupunguza kama si kumaliza kabisa kasi ya sasa ya matukio ya rushwa ya ngono katika shule na vyuo.

Licha ya kupongeza jitihada zinazoendelea kuchukuliwa hususan ya kutoa elimu ya rushwa shuleni, tunazishauri shule zote pamoja na vyuo kutekeleza mpango huo kwa kuwa utasaidia kuongeza uelewa wa watoto na wanafunzi kuhusu rushwa na athari zake kwao hususan ya ngono ambayo imekithiri na kuwaathiri ktika maeneo yao ya masomo.

Matarajio yetu ni kuwa tunaweza kuwa na jamii yenye uelewa mpana kuhusu rushwa, hivyo wengi kuichukia katika jamii na mwishowe janga hilo kupungua kwa kiwango kikubwa katika jamii, hivyo nchi kupaa kimaendeleo katika siku za usoni.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Yasmine Protace

## Muungwana Lazima Nilonge

# Hili la kutapisha maji machafu msimu wa mvua linakera sana

UMETIMU msimu wa mvua na sasa unaendelea katika baadhi ya mikoa nchini. Nianze kusema ni neema kwa wakulima na sote, maana chakula ni muhimu kwa kila mmoja wetu, wakati huohuo mvua ina umuhimu sana kwa mengi ya kimazingira, pia 'maji ni uhai.'

Pamoja na mvua hizo kuendelea kunyesha kila mahali, baadhi ya watu wana mapokeo yake katika sura hasi wakitaja ndugu zetu wengi wa mijini na mfumo yao ya vyoo si sahihi.

Mvua zinaponyesha na vyoo vyao kufurika, mbinu wanayotumia ni kujaribu kutiririsha maji hayo machafu mtaani katika namna maarufu kwa jina la 'kuyatapisha.'

Nafuu hiyo, inazua lingine la uchafu umma jirani unasambaziwa maji hayo yenye vinyesi.

Tahadhari ya afya ambayo ni angalizo la awali, ni kwamba wanaotapisha maji hayo machafu, wajue wazi kuwa wanasababisha kuwapo kwa milipuko ya magonjwa hata ikiwamo watu kuhara ovyo.

Inakera kuona mtu anaona shida kutafuta gari za majitaka ili kunyonya maji hayo, anahamia mbadala wa kuwachukua na kuwalipa fedha kidogo mfano kati ya Sh. 5000 na Sh. 10,000, wamfanyie kazi ya 'kutapisha choo chake.

Ieleweke kwamba inapofanyika hivyo, kuna maana kwamba wanavyotapisha maji hayo yanaenda mitaani wanakoishi watu wengine wakubwa kwa wadogo, wenye viatu na wasio navyo, wakubwa kwa wadogo baadhi wanayakanyaga na watoto hata kuhusisha na mikono na midomo yao.

Tukumbuke, kuna watoto mitaani wadogo hupenda kuchezea maji hata mvua zikinyesha na kukatika. Sasa hao watoto wanapochezea maji hayo, nao ndio wa kwanza kunaangukia magonjwa hatari ya kuambukiza kama kuhara na kutapika.

Hivyo, muhimu ninaloliona ni kwamba, sote tuwe wastaarabu kuwajali watu wote, kwa kila namna tunavyoweza na mojawapo lipo dhahiri ni hilo la kutasambaza maji machafu kwa makusudi.

Mara zote, magari ya kuchukua maji taka yapo mengi na la busara hapo ni kuwapo utaratibu binafsi au wa kifamilia, kuweza kuyatoa majitaka kwa njia iliyo sahihi na sio kuyafungulia njia, ili yaende kwa wenzako.

Pia ifahamike umma wote unatumia mvua hiyo katika maeneo yao, yakivuka sehemu mbalimbali za mtiririko wake.

Kukabili afya ya mazingira inaanza na namna kila mtu anavyojua miundombinu ya maeneo yako yalivyo, kisha wanayaweka vizuri, ili mvua zikinyesha zisiweze kuleta athari kwa wengine.

Najua kuna taarifa zinazitolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa, ikifafanua kila kitu kuhusu ujoo wa mvua na mwenendo wake, hali ya hewa kila juu wa mvua na jinsi ya kujianda au kujihadhari mapema.

Hatua za kuchukua mapema inaanzia pamoja na kuweka vizuri miundombinu, ili mvua zinapoanza kunyesha mtu asipate shida kwenye mwanzo wake.

Cha kushangaza mvua zinaponyesha tu, mtu akiona maji yamejaa kwake, badala ya kufanya utaratibu unaofaa, yeye anachokimbilia ni kuyaelekeza maji yaende katika nyumba ya mwenzake au kwingineko, bila kujali huko kuna umma.

Huyo anayefanya hivyo, anamsababishia mwenzake nyumba yake kujaa maji na aingie gharama za kuyatoa maji tena machafu.

Niseme, kinachotakiwa hapo ni watu waishi kwa upendo na ushirikiano na daima sio busara mtu kuelekeza maji ya mvua kwa makusudi yaingie katika nyumba ya mwenzake asoyr na kosa, hali ambayo hata inakinzana na kanuni, sera pia sheria za mazingira.

Kama wewe huyapendi maji hayo yakae kwako, basi nawe usimpelekee mwenzako maji hayo kama tunavyofunzwa kiimani na kijamii, usichopenda kutendewa wewe, usimtendee mwenzako.

HABARI KITAIFA




Mwenyekiti wa Bodi ya MIC Tanzania PLC, Rostam Aziz, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akijitambulisha rasmi kuwa mmoja wa wabia wa kampuni hiyo inayomiliki kampuni ya simu ya Tigo Tanzania. Kushoto ni Mwenyekiti wa Kampuni ya Axion na mbia mwenza wa kampuni ya Tigo, Hassanein Hirdjee. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAMWA: Sheria Habari ishughulikie unyanyasaji waandishi wanawake

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MKURUGENZI wa Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), Dk. Rose Reuben, ameshauri maboresho ya Sheria za Habari kuingizwa suala la kushughulikia unyanyasaji wa waandishi wa habari wanawake ili kukabiliana na changamoto hiyo katika vyombo vya habari.

Dk. Rose alisema hayo kwenye mkutano wa wadau wa habari na serikali ulioandaliwa na Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania, MISA-TAN na TAMWA kwa ufadhili wa Shirika la Kimataifa la Kusaidia vyombo vya habari, IMS, wakilenga pamoja na mambo mengine kujadili mapitio ya Sheria za Habari.

Alisema waandishi wa habari wanawake wameendelea kupungua katika vyombo vya habari kutokana na changamoto mbalimbali kubwa likiwa ni unyanyasaji wa kijinsia.

Alishauri vyombo vya habari kuwa na sera ya usawa wa jinsia ili kusaidia kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazoendelea katika vyombo hivyo.

Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO), Gerson Msigwa, alisema suala la unyanyasaji waandishi wa habari wanawake linashughulikiwa na ofisi yake na kuahidi kuweka dawati maalum la jinsia kukabiliana na changamoto hiyo.

"Unyanyasaji wa kijinsia haukubaliki ni kinyume cha sheria za nchi, tutaendelea kushirikiana na vyombo vya habari kuboresha sheria mbalimbali zinazokwaza uhuru wa habari," alisema Msigwa.

Aliwapongeza waandishi wa habari wa Tanzania ambao licha ya wengi wao kukabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo kutolipwa au kukosa mishahara, bado hawajarudi nyuma katika kutimiza majukumu yao ya kuhabarisha umma.

"Niwaahidi tu hakuna jambo litakwama ndani ya Serikali ya awamu ya sita, labda tuamue wenyewe (wanahabari) kuanzisha chokochoko zenye nia ovyo na kuharibu hali ya hewa," alisisitiza Msigwa.

Mwenyekiti wa TAMWA, Joyce Shebe, alisema vyombo vya habari nchini bado vinakabiliwa na changamoto ya unyanyasaji dhidi ya wanawake, sheria kandamizi na ukosefu wa maslahi bora kwa wanahabari.

Naye Mwenyekiti wa MISA Tanzania, Salome Kitomari, alisema pamoja na mambo mengine, mkutano huo wa pili licha ya kulenga kushauriana na serikali na wadau wengine masuala hayo ya kisheria yamelenga pia kujadili usalama wa waandishi wa habari katika vyombo vya habari.

Mengine ni kuangalia sera na sheria zinazominya uhuru wa vyombo vya habari na mazingira ya Tanzania, masuala ya unyanyasaji wa kijinsia na rushwa ya ngono katika vyombo vya habari na kupata mrejesho wa mapendekezo ya uwakilishi wa timu maalum ya majadiliano itakayoshughulikia marekebisho ya sheria za habari kama alivyoagiza Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia, Nape Nnauye.

Makamu Mwenyekiti wa MISA TAN, Wakili James Marenga, alisema bado kuna upungufu kadhaa katika Sheria za Habari nchini ikiwamo kugeuzwa makosa ya wanahabari ya kitaaluma kuwa makosa ya jinai na vifungu kadhaa vinavyokinzana na Ibara ya 18 ya Katiba ya nchi.

# Wakurugenzi kikaangoni, rungu kutua kwa ma-RAS

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, amewaweka kikaangoni wakurugenzi wa halmashauri 37 baada ya kuwataka kujieleza kwanini wasitumbuliwe kwenye nafasi zao kutokana na kuonyesha utendaji kazi usioridhisha katika vigezo sita vilivyowekwa ikiwamo ukusanyaji wa mapato.

Wakurugenzi watano kati ya hao ni wa Halmashauri za Bunda, Kigoma, Serengeti, Bumbuli na Nkasi na Makatibu Tawala wa Mikoa yenye halmashauri hizo zilizopata alama za chini katika tathmini ya ufanisi wa utendaji, wote wanapaswa kuandika barua ya kujieleza kwanini yasitolewe mapendekezo ya kutengua nafasi zao kwa Rais.

Pia, wakurugenzi 32 ambao halmashauri zao zimepata alama zisizoridhisha, wanapaswa kuandika barua kwa Katibu Mkuu TAMISEMI kujieleza kwanini waendelee kuaminiwa katika nafasi walizonazo.

Akitoa taarifa ya mapato na matumizi ya ndani ya halmashauri kwa kipindi cha robo tatu ya mwaka wa fedha wa 2021/22 (Julai 2021 hadi Machi 2022) jijini hapa jana, Waziri Bashungwa alisema vigezo sita vilivyotumika kwenye tathmini hiyo ni ukusanyaji wa mapato ya ndani, namna walivyojibu hoja za ukaguzi, matumizi ya mapato ya ndani katika miradi ya maendeleo, utoaji wa mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani na usimamizi wa urejeshaji wa mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani.

Alisema kwa ujumla tathmini ya utendaji kazi wa halmashauri ni asilimia 70 ambapo halmashauri 24 zimefanya vizuri kwa kupata alama kati ya 81-100, halmashauri 38 zimepata alama kati ya 75-80, halmashauri 90 zimepata alama 61-74 na halmashauri 32 zimepata alama kati ya 21-60.

"Kwa zile halmashauri 32 ambazo zimepata alama zisizoridhisha, nataka wakurugenzi wa halmashauri waandike barua kwa Katibu Mkuu TAMISEMI kwanini tuendelee kuwaamini katika nafasi zao, nataka ifikapo Mei 13, kila mkurugenzi awe ameandika barua kutokana na utendaji usioridhisha," alisema.

Alimwagiza Katibu Mkuu kufikia Mei 13, mwaka huu kwa wakurugenzi wa halmashauri tano zilizopata alama hizo za chini wawe wameandika barua kupitia kwa Katibu Mkuu TAMISEMI kwanini asipendekeze kwa Rais watenguliwe nafasi zao.

"Sambamba na hili nataka Makatibu Tawala wa Mikoa kwenye hizi halmashauri nao wajieleze kufika Mei 13, mwaka huu, kwanini nisipendekeze kwa Rais wasitenguliwe kwenye nafasi zao," aliagiza.

**ZILIZOFANYA VIZURI**

Alisema halmashauri tano zilizoongoza kwa kupata daraja A ni Halmashauri ya Mji wa Mbulu ikifuatiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Babati, Mtwara, Ludewa na Songea na kuagizwa waitwe kupata pongezi.

Kutokana na tathmini hiyo, Bashungwa alisema TAMISEMI ilishaanza kuchukua hatua ikiwa ni pamoja na kuwabadilisha vituo baadhi ya wakuu wa idara na vitengo kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi.

Alitolea mfano Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imefanya marekebisho pasipo kuwa na vithibitisho ya Sh. bilioni 10.86 na Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela iliyofanya marekebisho bila vithibitisho yenye thamani ya Sh. bilioni 8.72 kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za

halotel

TAARIFA KWA UMMA

Viettel Tanzania PLC (Halotel) ni kampuni ya mawasiliano inayoendelea kuboresha huduma na kuvunja mipaka ya mawasiliano kwa wateja wetu kwa kutoa gharama nafuu kwenye SMS, Huduma za kupiga simu na Intaneti.

Tunapenda kuwatangazia wateja wetu na umma kwa ujumla juu ya gharama zetu za makato pindi mteja atakapokuwa hajajiunga kwenye kifurushi.

GHARAMA ZA NDANI YA NCHI

| Kipengele | Gharama |
|---|---|
| Kupiga Halotel kwenda Halotel | 30 Tsh/Dk |
| Kupiga Halotel kwenda mitandao mingine | 30 Tsh/Dk |
| Kutuma SMS | 5 Tsh/SMS |

GHARAMA ZA NJE YA NCHI

GHARAMA ZA KUPIGA SIMU NJE YA NCHI

| Kanda | Gharama (Tsh/Dk) |
|---|---|
| **Ukanda 1:** USA, UK, India, China, Canada, Australia, Japan, South Korea, Vietnam, Laos, Cambodia | 450 |
| **Ukanda 2:** Nchi nyingine za ULAYA, Kenya | 750 |
| **Ukanda 3:** Rwanda, Afrika Kusini, Zambia, UAE, Oman,Haiti, Peru | 840 |
| **Ukanda 4:** Cameroon, Zimbabwe, Malawi, Uganda, Congo DRC, Mozambique | 1,000 |
| **Ukanda 5:** Burundi | 1,350 |
| **Ukanda 6:** Sehemu nyingine duniani | 2,700 |
| **Ukanda 7:** Mitandao ya satelite | 13,800 |

GHARAMA ZA KUTUMA SMS NJE YA NCHI

| SMS | Gharama |
|---|---|
| SMS kwenda nje ya nchi | 95 Tsh/SMS |

GHARAMA ZA INTANETI

| Data (MBs) | Gharama |
|---|---|
| Data | 9.35 Tsh/MB |

Halotel Tanzania

Hotline 100

# Mradi wa bil. 5.5/- kumaliza tatizo la majisafi Mkuranga

**Na Mwandishi Wetu**

MRADI wa maji safi utakaogharimu Sh. bilioni 5.5 unatarajiwa kuwaondolea kero ya maji wananchi wa Mkuranga na Vikindu mkoa wa Pwani.

Mkurugenzi wa Miradi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Mhandisi Ramadhani Mtindasi, alisema hayo jana wakati wa hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi kwenye mradi huo uliofanywa na Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa, Sahili Geraruma

Alisema kwenye mradi huo wanatumia chanzo cha maji chenye kina cha mita 545 ambacho kina uwezo wa kuzalisha maji lita 284,400 kwa saa.

Mhandisi Mtindas aliongeza kuwa lengo la mradi ni kukabiliana na changamoto zote zinazowakumba wakazi wa Mkuranga zinazotokana na shida ya majisafi ikiwemo magonjwa.

"Pia mradi umehusisha uwekaji wa mtandao wa kusambaza maji kwa kutumia mabomba ya inchi 2 hadi inch 8 kwa umbali wa kilomita 65," alisema

Mhandisi Mtindasi alisema wanajenga kituo cha kusukuma maji kutoka kwenye chanzo hadi kwenye tenki kwa umbali wa kilomita 1.3. "Uwepo wa mradi huu ni faida kwa wakazi kwani utaleta majisafi na kusaidia kupunguza magonjwa ya mlipuko katika maeneo yote na kuboresha usafi wa Mazingira," alisema.

Mtindasi alitoa shukrani kwa serikali kwa kuona umuhimu wa mradi huo na kutoa fedha kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa mradi kwa kasi.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Geraruma alisema amеridhika na utekelezaji wa mradi huo na kwamba utanufaisha wakazi wengi wa Mkuranga na maeneo ya jirani.

"Nimekagua kazi zote zilizofanyika kwenye mradi ikiwemo ujenzi wa chanzo cha kuzalisha maji chenye uwezo wa kuzalisha lita 284,400 kwa saa, pamoja na tenki la kuhifadhi maji Mkuranga lenye ujazo wa lita milioni 1.5," alisema.

"Rais Samia Suluhu Hassan anawapenda wakazi wa Mkuranga na ndiyo maana amewezesha mradi huu kutekelezwa kwa kasi ili kumtua mama ndoo ya maji kichwani," alisema Geraruma.

Aliitaka DAWASA kuhakikisha huduma ya maji inakua endelevu na wananchi wanapata majisafi muda wote.



Wafanyakazi wa kampuni ya Sukari ya Kilombero, wakiwa kwenye maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani, yaliyofanyika kimkoa katika viwanja vya CCM Tarafa ya Mikumi, wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC asifu kiwanda kutenga mamilioni kuisaidia jamii

**Na Mwandishi Wetu,** KILOSA

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela, ameupongeza uongozi wa Kampuni ya Sukari ya Kilombero kwa uamuzi wake wa kutenga fedha zinazotokana na mapato ya kila mwaka kwa ajili ya kuimarisha huduma za jamii katika maeneo ya vijiji vinavyozunguka kiwanda hicho.

Shigela alitoa pongezi kwa kiwanda hicho wakati wa mkutano wa hadhara na wananchi wa Kata ya Ruaha, Tarafa ya Mikumi wilayani Kilosa uliofanyika juzi, ukiwashirikisha pia baadhi ya viongozi wa Kiwanda cha Sukari Kilombero.

Katika mkutano huo, baadhi ya wananchi waliwasilisha kero kadhaa zinazowakabili zikiwamo za ubovu wa miundombinu ya barabara, ukosefu wa huduma bora za afya, maji na ofisi za kutolea huduma za jamii.

"Niupongeze uongozi wa Kampuni ya Sukari ya Kilombero kwa hatua hii kwani jambo hilo litaimarisha uhusiano mwema uliopo kati ya kiwanda na wananchi wa maeneo ya vijiji na kata zilizopo ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa pamoja na ya Kilombero ambao wamepitiwa na maeneo ya kiwanda hiki," Shigela alipongeza.

Mkurugenzi wa Idara ya Uhusiano ya Kampuni ya Sukari ya Kilombero, Ephraim Mafuru, baada ya kujitokeza kwa kero hizo, alisema kuwa kiwanda kitatenga fedha zaidi ya Sh. milioni 400 kila mwaka kwa ajili ya kuimarisha huduma za jamii.

Alisema fedha hizo zitatumika kuimarisha huduma za jamii katika maeneo yanayozunguka kiwanda hicho na wale ambao wanapakana na mashamba ya miwa ya kiwanda.

Mafuru alisema wananchi wa maeneo hayo wamekuwa na mchango mkubwa katika uendeshaji wa kiwanda na fedha hizo zinastahili kuimarisha miundombinu katika maeneo yao ikiwa ni sehemu ya kutambua mchango wao kwa kiwanda hicho.

Katika hatua nyingine, Uongozi wa kiwanda hicho umeahidi kuweka kipaumbele cha ajira kwa wananchi wa maeneo yanayozunguka kiwanda katika mradi wake wa upanuzi ambao utekelezaji wake unatarajiwa kukamilika mnamo Julai 2024.

Kampuni ya Sukari ya Kilombero pia imeendelea kuboresha huduma za ustawi kwa wafanyakazi wake kwa kujenga zaidi ya nyumba 1,800 kwa ajili ya makazi.

Meneja Masuala ya Biashara wa Kiwanda hicho, Bruno Daniel, alibainisha hayo juzi katika viwanja vya CCM Tarafa ya Mikumi wilayani Kilosa.

Pia alisema kwa wafanyakazi wanaoishi nje ya kambi, wanapewa asilimia 15 ya mishahara yao kwa ajili ya kufidia gharama za makazi.

## Wazazi wahamasishwa umuhimu chanjo ya polio

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

WANANCHI mkoani Ruvuma wamehimizwa kuona umuhimu wa kuwapeleka watoto wao kupata chanjo za ugonjwa wa polio.

Kauli hiyo ilitolewa jana na mratibu wa chanjo mkoani Ruvuma, Winbroad Mvule wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ugonjwa huo ambao husababisha kupooza.

Mvule aliwakumbusha wazazi wenye watoto chini ya umri wa miaka mitano kuwa chanjo wanaoendelea kupatiwa watoto wao hazitawaathiri na kwamba ni muhimu wawapeleke watoto wao wakapatiwe chanjo hiyo kwa awamu zote nne kama ilivyoelekezwa na serikari kupitia Wizara ya Afya.

Mratibu wa chanjo mkoani Ruvuma, ameitaka jamii ya wana-Ruvuma kuwahamasisha wote ambao wataonekana kupinga watoto wao kupatiwa chanjo kuwa endapo mmoja ya watoto miongoni mwao asipochanjwa ni rahisi ugonjwa ukiingia kuwa na uwezekano wa kusambaa kwa watoto wengine na kuitaka jamii kusaidia kutoa elimu ambayo inaweza kuleta kinga ya ugonjwa huo.

Alifafanua kuwa chanjo ya kwanza ilitolewa Machi 24 mpaka 27, mwaka huu na zaidi ya watoto 293,543 walipatiwa chanjo hiyo sawa na asilimia 122 na watoto waliotarajiwa kufikiwa katika mpango ni 241,966, lengo lilifikiwa kutokana na mwamko wa wananchi walioupata kupitia elimu iliyotolewa na hamasa katika jamii.

Kutokana na hamasa iliyopatikana katika awamu ya kwanza, mratibu huyo aliitaka jamii kujitokeza kwa wingi wazazi kuwapeleka watoto wao kupata chanjo ya awamu ya pili ili kuendelea kuwakinga.

Chanjo kwa awamu ya kwanza ilihusisha mikoa minne iliyo jirani na Malawi ambayo ni Ruvuma, Iringa, Songwe na Mbeya na katika awamu ya pili chanjo hiyo itatolewa kwa nchi mzima kwa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano.

## Zimamoto yaweka mkazo kwenye elimu

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

KATIKA juhudi za kupunguza na kutokomeza majanga ya moto, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani Iringa linaendelea na utoaji elimu juu ya kinga na tahadhari dhidi ya majanga ya moto.

Elimu hiyo inatolewa katika maeneo ya majumbani, maeneo ya kazi na vyombo vya moto.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa maadhimisho ya Wiki ya Zimamoto na Uokoaji jana, Kamanda wa Jeshi hilo Mkoa wa Iringa, Mrakibu Isabela Mbwago, alisema kuwa jeshi lina jukumu la kutoa huduma kwa jamii katika nyanja mbalimbali zikiwamo kuokoa maisha ya watu na mali zao.

Kamanda huyo alitaja baadhi ya majukumu hayo ambayo jeshi linafanya kuwa ni kuzima moto, kutoa elimu ya kinga na tahadhari ya majanga moto, kufanya ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto, kusoma ramani za majengo na kutoa ushauri.

Mbwago aliongeza kuwa jeshi hilo pia linatoa huduma ya kwanza katika majanga ya ajali barabarani, kutoa mafunzo ya kukabiliana na majanga ya moto, kufanya uchunguzi kwenye majanga ya moto na kutoa huduma za kibinadamu.

"Huduma ya Zimamoto inatolewa bure na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji hivyo basi tunawaasa wananchi kutumia namba ya dharura 114 mara tu wapatwapo na majanga ili kurahisisha uokoaji wa maisha na mali kwa haraka," alisema Mbwago.

Mbwago alizundua wiki ya maadhimisho hayo kwa kufanya ukaguzi wa magari katika stendi ya mabasi yaendao vijijini ya mjini Iringa na Mlandege na kujionea mapungufu kwenye magari yao kama vile kutokuwa na vifaa vya zimamoto.

Mengine ni kwamba wafanyakazi wengi ambao wanafanya kazi katika magari hayo hawajui matumizi ya namba ya dharula ya 114 ya zimamoto ya kupiga majanga yanapotokea, hivyo kuwataka wenye magari kufanya marekebisho ya mapungufu hayo yote na walete magari yao yakaguliwe bure katika pindi hiki cha wiki ya maadhimisho.

Kaulimbiu ya maadhimisho hayo mwaka huu 2022 ni 'Uchumi imara kwa kuzingatia kinga na tahadhari dhidi ya majanga ya moto,' na kilele cha maadhimisho hayo ni Ijumaa Mei 5, 2022.

Mbwago aliwataka wananchi mkoani Iringa kujitokeza kwa wingi katika wiki ya maadhimisho ili wapate elimu ya tahadhari ya moto na pia wapeleke magari yao yakaguliwe bure pamoja na kuwaonesha jinsi ya kutumia vifaa ya kuzimia moto kwenye magari.

# Wakulima watishiwa uhai na tembo wilayani Tunduru

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

TEMBO wamekuwa tishio kwa mazao ya wakulima sambamba na kutishia maisha ya wakazi wa Wilaya ya Tunduru.

Mkazi wa Kijiji cha Marumba Kata ya Marumba wilayani Tunduru mkoani Ruvuma, Sheikh Alumba Amanzi Kalengo (67), ameuawa na mnyama huyo.

Katengo alikutwa na madhila hayo baada ya kushambuliwa na mnyama huyo alipokuwa anakwenda kwenye Swala ya Eid el Fitri.

Taarifa zinaeleza kuwa tukio hilo lilitokea juzi majira ya asubuhi akiwa anatokea katika eneo la mashamba ya kijiji cha Mishyaje umbali wa kilometa moja kuingia kijiji cha Marumba baada ya kukutana na kundi la tembo hao waliokuwa katika eneo la bwawa la Mto Namasimba.

Diwani wa Marimba, Said Makunganya, alisema Kalemgo alikuwa mkazi wa kitongoji cha Tujuwane katika kijiji cha Marumba na kwamba katika tukio hilo siku hiyo alilala shambani kwa ajili ya ya ulinzi wa tembo ambao kwa sasa wanavamia mashamba na kula mazao ya wakulima.

Diwani wa Viti Maalum Tarafa ya Nalasia, Aindi Daruweshi, alisema kuwa kwa sasa matukio ya tembo katika tarafa hiyo ni ya kawaida, hali ambayo imekuwa ni kero kubwa ambayo ilipelekea baadhi ya wakazi wa Kata ya Mbati kufanya vurugu za kuchoma ofisi za serikali na baadaye kuua tembo mmoja wakiwa wanashinikiza serikali kuangalia uwezekano wa kuondoa wanyama hao.

Kufutia hali hiyo, viongozi hao wameiomba Wizara ya Maliasili na Utalii kuangalia uwezekano wa kuwatembelea wakazi wa maeneo hayo ili kutoa elimu ya kujikinga na wanyama hao waharibifu na kuona namna ya kuwafidiwa mazao yao na kuwafanya waweze kujikimu na familia zao ili wasikumbwe na baa la njaa.

Ofisa Wanyamapori wa Wilaya ya Tunduru, Limbega Ally, alisema kuwa ameshapeleka askari wenye silaha kwa ajili ya kuwafukuza wanyama hao wasiendelee kusababisha madhara kwa wananchi.

Limbega alisema kuwa kwa mwaka huu hilo ni tukio la pili la mtu kuuawa na tembo.

Alisema hali hiyo imetokana na kusambaa kwa wanyama hao kwa wingi katika maeneo ya makazi ya wananchi.

Limbega aliwapa angalizo wananchi kuacha tabia ya kuwafukuza tembo hao usiku ili kunusuru maisha yao na kwamba mazao wanayodai kuyapigania yanatafutwa hayawezi kulinganishwa na uhai wa binadamu.



Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Sahili Geraruma (wa tatu kushoto) akipata maelezo ya utekelezaji wa mradi wa maji Mkuranga - Vikindu kutoka kwa Mkurugenzi wa Uwekezaji na Miradi wa DAWASA, Mhandisi Ramadhan Mtindasi, wakati wa hafla ya kuweka jiwe la msingi kwenye mradi huo wilayani Mkuranga juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wasafiri sasa wahakikishiwa huduma za Bolt kuendelea

**Na Mwandishi Wetu**

WASAFIRI wanaotumia usafiri kwa njia ya mtandao wamehakikishiwa kuwa wataendelea kunufaika na huduma hiyo.

Ahadi hiyo imetolewa na kampuni ya usafiri kwa njia ya mtandao nchini ya Bolt, kwamba itaendelea na huduma za usafiri nchini kama kawaida.

Wadau wa usafiri huo wameondolewa wasiwasi huo kutokana na taarifa iliyochapishwa Aprili 20, 2022 na mtandao wa TechCrunch, yenye taarifa ya Bolt kuhusu hali ya biashara Tanzania kama matokeo ya agizo lililotolewa na LATRA Machi 14 .

Bolt Tanzania imesema imekuwa na mkutano wenye mafanikio na LATRA Aprili 27, 2022 ili kujadili zaidi suala hili.

Akizungumza kuhusu taarifa hiyo Meneja wa Bolt Afrika Mashariki, Kenneth Micah Reginald, amesema kutokana na mkutano walioufanya, wamepiga hatua kubwa katika kufikia suluhu la jambo hili na wanatarajia utatuzi wa haraka.

Kenneth alisema:"Bolt inapenda kusisitiza kwamba imejitolea kuendelea kutoa huduma za usafiri kwa soko la Tanzania, na kutengeneza fursa za ujasiriamali zinazowezesha watu wengi zaidi kujikimu kimaisha."

Kwa mujibu wa Kenneth, Bolt itaendelea na ushirikiano wake na wadau husika ikiwa ni pamoja na LATRA utatoa mapitio mazuri ya kanuni kuhusu ushuru, na uwekaji kamisheni kwa kampuni ya vyombo vya usafiri wa kukodi ili kuwezesha shughuli endelevu za kazi.

# Majalada kesi kongwe mauaji kuchunguzwa

WIZARA ya Katiba na Sheria, imeunda kikosi kazi kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai kupitia majalada ya kesi za mauaji zenye muda mrefu kuanzia miezi miwili na kuendelea.

Kikosi kazi hicho kinaendelea na kazi ya kupitia majalada ambapo kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi huu.

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Geoffrey Pinda, alisema hayo jana Bungeni jijini hapa na alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Lupembe (CCM), Edwin Swalle.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji mpango wa serikali katika kuharakisha mashauri ya kesi za mauaji ambazo watuhumiwa wengi wanakaa mahabusu muda mrefu bila kesi zao kusikilizwa.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri alisema wizara hiyo kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeunda kikosi hicho na majalada hayo yanafanyiwa mapitio na kutolewa uamuzi.

"Nimwombe Mheshimiwa Mbunge kuwa na subira ili kutoa muda hadi mwishoni mwa mwezi Mei, 2022, kesi zote za muda mrefu zitakuwa zimeshughulikiwa," alisema.

Katika swali la nyongeza, Swalle alisema watuhumiwa wengi wa mauaji wanakaa rumande kwa muda mrefu wakisubiri mashauri yao kusikilizwa huku wengine wakifia rumande wakisubiri kesi zao kusikilizwa.

"Kwa nini serikali isiteue mahakimu na majaji wasikilize mashauri haya kwa haraka? Kwa kuwa kesi za mauaji zinacheleweshwa kwa makusudi au bahati mbaya ni lini serikali italeta bungeni sheria ya ukomo kesi za mauaji ili upelelezi ukamilike?" Alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Pinda alisema pamoja na uhaba wa majaji uliopo, serikali imewaongezea mamlaka mahakimu wakazi katika mahakama mbalimbali ambazo hazina mamlaka ya kusikiliza kesi za mauaji.

Alisema mahakimu 153 wameongezewa mamlaka za kusikiliza kesi hizo na kwa upande wa mahakama hakuna ucheleweshaji wa kesi isipokuwa eneo la upelelezi ambalo tayari kimeundwa kikosi hicho ili kesi ziishe kwa wakati.

Alibainisha kuwa dhamira ya serikali ni kumaliza kesi hizo kwa wakati licha ya kuongezeka kila siku.



Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Geoffrey Pinda

# NEC kutangaza sifa za maeneo kugawanya majimbo ya uchaguzi



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Nderiananga

KATIKA maandalizi ya kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) itatangaza utaratibu na sifa za kugawa maeneo mbalimbali kwa ajili ya uchaguzi, Bunge lilielezwa jana mjini hapo.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Nderiananga, alisema hayo alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Makambako (CCM), Deo Sanga.

Mbunge huyo alihoji lini serikali itaangalia upya mipaka ya kiutawala katika Jimbo la Makambako.

Akijibu swali hilo, Nderiananga alisema kwa mujibu wa ibara ya 74(6)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, NEC ndiyo yenye dhamana ya kuchunguza mipaka na kuigawa katika majimbo ya uchaguzi kwa ajili ya uchaguzi wa wabunge.

"Hivyo, Mheshimiwa Mbunge anashauriwa kuwa pindi tume itakapotoa tangazo la kuanzisha maeneo mapya ya kiutawala, ashirikiane na mamlaka za kiutawala katika wilaya na mkoa kuandaa na kuwasilisha mapendekezo kwa kuzingatia vigezo vitakavyokuwa vimewekwa na tume," alisema.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alihoji lini utekelezaji wa suala hilo utafanyika kwa haraka.




Mbunge wa Makambako (CCM), Deo Sanga.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Nderiananga alisema maandalizi yanaendelea na wakati utakapofika Tume itatangaza na mbunge awasilishe maombi anayoomba.

# Maziwa makuu kutumika kumaliza tatizo la maji



Mbunge wa Nkasi Kaskazini, Aida Khenani




**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imepanga kutumia maziwa makuu kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi waishio karibu na vyanzo hivyo.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alisema jana bungeni jana alipokuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Nkasi Kaskazini (CHADEMA), Aida Khenani.

Katika swali lake, Khenani alihoji lini serikali itasambaza maji katika Wilaya ya Nkasi kutoka Ziwa Tanganyika.

Aweso, akijibu swali hilo, alisema kutokana na kuwapo tatizo la upatikanaji wa maji kwa njia ya visima katika maeneo ya maziwa, serikali imeamua kutumia maziwa makuu kuboresha upatikanaji wa huduma hiyo kwa wananchi waishio karibu na vyanzo hivyo wakiwamo wa Nkasi mkoani Rukwa.

"Katika kutimiza azma hiyo, serikali imeanza kutumia Ziwa Tanganyika kuwanufaisha wananchi wa wilaya ya Nkasi ambapo katika mwaka wa fedha 2021/22, serikali imekamilisha miradi ya maji ya Kirando-Kamwanda, Mkinga na mradi wa maji Kabwe," alisema.

Aweso alisema kukamilika kwa miradi hiyo kumeboresha hali ya upatikanaji wa huduma maji wilayani Nkasi kutoka asilimia 47 hadi asilimia 53.

Kwa mujibu wa Aweso, katika mwaka wa fedha 2022/23, serikali itaendelea na usanifu wa miradi ya maji kupitia chanzo cha Ziwa Tanganyika kwenye vijiji 10 vya Kilambo, Kala na Tundu (Kata ya Kala), Izinga, Mwinza na Wampembe (Kata ya Wampembe), Ninde, Kisambala na Namasi (Kata ya Ninde) na Mandakerenge (Kata ya Kipili).

Pia alisema katika mwaka 2022/23, usanifu utafanyika kwa ajili ya kupeleka maji katika mji wa Namanyere pamoja na vijiji vilivyoko kilomita 12 kila upande ambapo bomba kuu litapita na usanifu huo unatarajiwa kukamilika katika robo ya pili ya mwaka wa fedha2022/23 na baadaye ujenzi utaendelea.



Waziri wa Maji, Jumaa Aweso

Katika swali lingine la msingi, Mbunge wa Viti Maalumu (CCM), Martha Mariki, alitaka kujua ni lini serikali itatekeleza mpango wa kutoa maji Ziwa Tanganyika na kuyapeleka mkoa wa Katavi.

Akijibu swali hilo, Aweso alisema hali ya huduma ya upatikanaji wa maji Mkoa wa Katavi ni asilimia71 kwa vijijini na asilimia 60 kwa mjini.

Alisema katika kuboresha huduma ya maji, serikali imeanza kutekeleza miradi ya maji kwa kutumia chanzo cha Ziwa Tanganyika.

Alisema katika mwaka wa fedha 2021/22 mradi unaoendelea kutekeleza ni mradi wa maji Karema katika wilaya ya Tanganyika utakaohudumia vijiji vya Kapalamsenga na Songambele (Kata ya Kapalamsenga), Isengule na Shukula (Kata ya Isengule) na unatarajiwa kukamilika Septemba, mwaka huu.

Pia alisema katika mwaka wa fedha 2022/23, serikali itaajiri mtaalamu mshauri wa kufanya usanifu wa kina wa ujenzi wa miundombinu wa chanzo cha maji chenye uwezo wa kuzalisha maji mengi kutoka Ziwa Tanganyika na kusaidia wananchi wa wilaya za Tanganyika, Mlele, Mpanda na maeneo ya karibu kunufaika na chanzo hicho.




Wakati mwafaka madaktari watumie ving'ora, vimulimuli

BUFE
IJUMAA MEI 6, 2022
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



## Wavuvi Mwanza walia thamani ya sangara imeshikwa na wanunuzi kupitia 'mabondo'

Ukurasa 14

MAPAMBANO YA RUSSIA VS UKRAINE

# Ni vita vikali kugombea Mariupol mji kiuchumi, kiwanda cha chuma

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kasi ya vita, Russia inatajwa kuingia kwenye kiwanda cha kutengeneza chuma cha Azovstal, kinachomiliki kikosi cha mwisho cha wanajeshi wa Ukraine kushika hatamu katika mji wa bandari wa Mariupol, Kusini mwa nchi hiyo.

Kwanini panabanwa? Daraja la ardhini: Russia inapigania, kudhibiti daraja la ardhini kutoka kwao, kupitia sehemu za mkoa wa Donbas unaoshikiliwa na watu wanaotaka kujitenga na wanaungwa mkono na Russia.

Pia, inalenga kuathiri uchumi wa Ukraine, kwani Mariupol kwa muda mrefu imekuwa bandari muhimu kimkakati kwenye Bahari ya Azov, sehemu ya Bahari Nyeusi.

Katika nyakati za kawaida, jiji hilo ni kitovu muhimu cha mauzo ya nje ya vyuma vya Ukraine.

Kiwanda cha vyuma cha Azovstal, kimepewa kipaumbele na uongozi wa kisiasa, pamoja na kijeshi wa Ukraine na Mshauri wa Waziri wa Ulinzi, Yuriy Sak, anasema juhudi zililenga kutetea eneo kubwa la viwanda na kudhibiti zaidi.

Azovstal ndiyo eneo la mwisho linaloshikiliwa na Ukraine katika mji wa kimkakati wa bandari ya Mariupol - ambao Sak anabainisha kuwa umekuwa 'moyo' wa vita.

Anaikiri, hali katika kiwanda hicho imekuwa ngumu sana, wapiganaji wa Russia sasa walishaanzisha mashambulizi ya ardhini, wakiwa wanatekeleza zaidi mashambulizi ya angani na makombora.

"Tuna matumaini kimya kimya," anasema Sak na kufafanua: "Lakini kwa kweli tumezoea Russia kutoheshimu ahadi zake."

Kwa upande wake, Russia awali ililaumu Ukraine kwa kuvunja makubaliano na kusababisha njia kupeleka misaada kufungwa huko Mariupol.

Bandari hiyo muhimu ya kimkakati, kwenye bahari ya Azov, imekuwa kwa njia nyingi ishara ya upinzani wa Ukraine dhidi ya uvamizi wa Russia.

Kwa wiki kadhaa, hatua ya mwisho ya upinzani huo imekuwa juhudi za kulinda kiwanda cha chuma cha Azovstal.

Baada ya siku kadhaa za mashambulizi makali ya mabomu, inaonekana Russia sasa imefanikiwa kufika eneo hilo, huku kamanda wa wanajeshi wa Ukraine ndani ya mtambo huo, akikiri kwa kauli "vita ni vikali vya umwagaji damu."

Kuteka jiji hilo ni namna inayoweza kuvipa vikosi vya Russia daraja la ardhini, kutoka eneo lao hadi kuliko jirani, kunakoitwa Crimea.



Sehemu ya kituo kilichoharibiwa katika kiwanda cha chuma cha Azovstal huko Mariupol juzi. **PICHA: MTANDAO.**

Baada ya muda, kikaripotiwa vikosi vya Russia vimeweza kuingia ndani ya kiwanda cha Azovstal huko Mariupol na kuna uwezekano kikatekeleza mashambulizi yake katika eneo hilo, kwa mujibu wa Taasisi ya Utafiti wa Vita (ISW) ya Marekani, katika tathmini yake ya hali ya kijeshi ya juzi.

Habari hizo zinajiri baada ya siku kadhaa za mapigano makali kwenye kiwanda hicho, ambako wapiganaji wa mwisho wa Ukraine katika mji huo wamekuwa wakipadhibiti, pamoja na mamia ya raia.

Taasisi hiyo yenye makao yake makuu nchini Marekani, pia inasema ulinzi wa Ukraine kwa kiasi kikubwa umezuia hatua zilizopigwa na wapiganaji wa Russia Mashariki mwa Ukraine.

Vikosi vya Ukraine hadi sasa vimezuia vikosi vya Russia kuunganisha mashambulizi yao Kusini Mashariki mwa Izyum na Magharibi wa eneo la mapambano mjini Donetsk-Luhansk.

Magharibi mwa Ukraine kuna majaribio ya vikosi vya Russia kuvuruga usafirishaji misaada kwenda Ukraine kutoka nchi za Magharibi.

Vikosi vya Russia vinatajwa kuzidisha mashambulizi ya anga dhidi ya miundombinu ya usafiri karibu na vituo vya reli huko Lviv na Transcarpathia wiki iliyopita, hatimaye vilishindwa kusababisha madhara makubwa.

**Kwa mujibu wa BBC.**

UCHUMI

# Ushuhuda mikopo halmashauri inavyobadili maisha ya wenye ulemavu kuibuka kiuchumi

## • Miradi vikundi yang'ara, mfukoni nako 'hapajambo'
## • Aliyetaabika kulea, sasa anamsomesha chuo kikuu

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

SERIKALI kupitia halmashauri, imekuwa ikitoa fedha za mikopo isiyo na riba kwa makundi ya wanawake, vijana na wenye ulemavu, wakijiunga kwenye vikundi vya ujasiriamali na kufanya shughuli za kuwaingizia kipato wajikwamue kiuchumi.

Mikopo hiyo imekuwa ikitolewa kwa wanawake na vijana, asilimia nne kila moja, huku wenye ulemavu wakipatiwa asilimia mbili.

Taarifa ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ya mwaka 2012, inasema asilimia 10 ya Watanzania ni wenye ulemavu, ambao ni milioni 4.4, wakiwa katika mgawanyiko, asilimia 9.4 wanawake na asilimia 9.1 wanaume.

Watu wenye ulemavu idadi yao kubwa wanakabiliwa na ugumu wa maisha, kwa sababu ni wategemezi na wanaopewa misaada, hata wanapopatiwa fursa, hawamudu kutumia.

Serikali sasa imeyakumbuka makundi hayo maalumu na kuanza kuyapatia mikopo, hata wengi wao kuitumia mikopo hiyo vyema, ikiwaengua kutoka kwenye umasikini, hadi kwenye maisha mazuri, baadhi wakisomesha watoto wao hadi ngazi ya vyuo.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, akiangalia bidhaa za vyakula vinavyotengenezwa na kikundi cha wanawake wenye ulemavu Amani, wanaojihusisha na utengenezaji vyakula. Kushoto, ni Mwenyekiti wa kikundi hicho Rehema Mkengele. **PICHA: MARCO MADUHU.**

### SIMULIZI ZA WAHUSIKA

Janety Limbe, ni mwanamke mwenye ulemavu wa macho anayeishi Kitangili katika Manispaa ya Shinyanga, mnufaika wa asilimia mbili ya mikopo ya halmashauri kupitia kikundi chao cha watu wenye ulemavu wanaojihusisha na ufugaji nguruwe.

Anasema, kupitia kikundi chao cha ufugaji nguruwe, mwaka 2019 walipata mkopo wa halmashauri Sh. milioni Mbili wakanunua nguruwe wawili na kuwajengea mabanda, hata nguruwe hao walizaliana mwaka jana wakapata mkopo wa Sh. Milioni tatu, zilizowawezesha kununua nguruwe 10.

Janety anaeleza mpaka sasa kikundi chao kina nguruwe 28 wenye watoto saba na wanapokuwa wengi, wana utaratibu kwamba huwa wanawauza na kugawana fedha wanazozitumia kwenye mahitaji ya nyumbani wakiwasomesha watoto, kwa kuwatimizia mahitaji ya shule na mmoja akimlipia chuoni.

"Kabla ya kuingia kwenye kikundi cha ujasiriamali cha watu wenye ulemavu na kupata mikopo hii ya halmashauri, nilikuwa nikiishi maisha magumu sana na kushindwa kuwatimizia mahitaji watoto wangu hasa ya shule kutokana na hali niliyonayo," anasema Limbe.

> **"Naishukuru serikali kwa kutoa fedha hizi za mikopo ya Halmashauri na kuyakumbuka makundi maalum na kwenda kutimiza ndoto zangu na kuja kuwasaidia wazazi wangu na wadogo zangu kuwaendeleza kielimu," anasema Michael.**

"Sasa hivi mimi siyo maskini tena kama zamani, sababu nina uwezo wa kuwahudumia watoto wangu ambao ninao sita na kuwatimizia mahitaji yao ya shule. Mmoja ninamlipia ada ya shule, ambaye anasoma ngazi ya stashahada katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi.

"Tunaiomba serikali iendelee kutoa fedha hizi za mikopo ya halmashauri, lakini iwe inatoa kiwango kikubwa cha fedha kulingana na tuliyoomba ili tukidhi mahitaji yetu.

"Mfano, mwaka jana kikundi chetu tuliomba Sh. milioni tano, lakini tukapewa milioni tatu fedha ambazo tulishindwa kukamilisha mipango yetu," anafafanua Janety.



Wenye ulemavu wa Shinyanga, wakiwa na baiskeli zao walizopewa, ziwarahisishie maisha na shughuli zao za kujikimu. **PICHA: MTANDAO.**

Pia, mwanafunzi Neema Michael, anayesoma kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Ibinzamata katika Manispaa ya Shinyanga, ni binti wa mama huyo mwenye shida ya macho, anasema awali walipata shida ya kutimizwa mahitaji yao shuleni, kutokana na hali ya mama yao, lakini sasa shida hiyo haipo tena.

Mtoto mwingine wa mama huyo, Ndiganya Michael, mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi ngazi ya stashahada, anasema fedha hizo za mkopo wa halmashauri zimemsaidia kutimiza ndoto zake, ambazo hakutegemea kuzifikia kutokana na uhalisia wa maisha nyumbani kwao.

"Naishukuru serikali kwa kutoa fedha hizi za mikopo ya Halmashauri na kuyakumbuka makundi maalum na kwenda kutimiza ndoto zangu na kuja kuwasaidia wazazi wangu na wadogo zangu kuwaendeleza kielimu," anasema Michael.

John Samweli ni mwanachama wa Kikundi cha Wenye Ulemavu cha Mapambano, wanaojihusisha na utengenezaji viatu vya ngozi na mwaka jana walipata mkopo kutoka halmashauri, Sh. milioni 10, hata maisha yao yamebadilika sasa kiuchumi, tofauti na ilivyokuwa awali.

"Tunaishukuru serikali kwa kutupatia mikopo hii ya halmashauri asilimia mbili, kwetu sisi watu wenye ulemavu ambayo imebadili kabisa mustakabali wa maisha yetu na sasa siyo tegemezi tena, bali tunaendesha maisha yetu na kuhudumia familia zetu ikiwamo kutimizia mahitaji ya shule kwa watoto wetu," anasema Samweli.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Shinyanga John Tesha, anasema halmashauri hiyo kati ya Julai na Desemba mwaka jana, wametoa fedha za mikopo Sh.milioni 175 kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga Jasinta Mboneko, anayasisitizia makundi ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu waendelee kuchangamkia fursa za mikopo ya halmashauri, wajikwamue kiuchumi.

Anayashauri makundi hayo yanapopokea fedha za mikopo ya halmashauri, yarejeshe fedha hizo kwa wakati uliokubaliwa, ili makundi mengine yaweze nayo kukopa, huku akiwapongeza wanawake na watu wenye ulemavu kuwa mastari wa mbele kurejesha fedha hizo kwa muda muafaka.

### MKUU WA MKOA AELEZA

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, anasema anafurahishwa na watu wenye ulemavu ambao wanachangamkia fursa za mikopo ya halmasahuri asilimia mbili na kufanya shughuli mbalimbali za ujasiriamali na kujikwamua kiuchumi.

"Wenye ulemavu wajiunge kwenye vikundi vya ujasiriamali, tena sasa hivi utoaji wa mikopo hii umeboreshwa, siyo lazima mjiunge watu wengi. Hata peke yako ukitimiza masharti unapata mkopo, nawaomba sana changamkieni mikopo hii ipo kwa ajili yenu," anasema Mjema.

"Vikundi vya watu wenye ulemavu ambavyo vimepata mikopo hiyo ya halmashauri asilimia mbili, naomba viwe mabalozi wazuri kwa wenzao na kuwapatia elimu namna jinsi wao walivyofanikiwa kupata mkopo na kuinuka kiuchumi," anaongeza Mjema.

### NAIBU WAZIRI

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Dk. Festo Dugange, akiwa mkoani Shinyanga kwenye kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, anatoa msisitizo kwa makundi ya wanawake, vijana na wenye ulemavu, wasiwe wazembe kuchukua fedha hizo za mikopo ya halmashauri, wajikwamue kiuchumi.

Pia, katika eneo hilo, anatoa maagizo kwa Wakurungezi na Maofisa Maendeleo wa Halmashauri zote nchini, kuwa fedha hizo za mikopo wawe wanazitoa nyingi kwa makundi machache ili kukidhi mahitaji yao na kuinuka kiuchumi, kuliko kutoa chache kwa makundi mengi, hata ikabaki kuendelea kujinasua toka kwenye umaskini.

"Naagiza Wakurugenzi wote wa Halmashauri, mikopo hii ya wajasiriamali ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, nataka iwe na tija kwao nani vyema mkavipatia vikundi vichache fedha nyingi, kuliko kutoa fedha kidogo kwa vikundi vingi na kushindwa kuinuka kiuchumi," anasema Dk Dugange.

### VYAMA VYA WALEMAVU

Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu mkoani Shinyanga (SHIVYAWATA), Richard Mpongo, anasema fedha hizo za mikopo za halmashauri, zimekuwa msaada mkubwa sana kwa watu wenye ulemavu kuwainua kiuchumi.

"Tunachoomba tu elimu ya ujasiriamali iendelee kutolewa zaidi kwa watu wenye ulemavu, ili waendelee kujiunga wengi kwenye vikundi na kupata mikopo," anasema Mpongo.

Hivi sasa mikopo ya halmashauri inatengwa asilimia 10 za bajeti; asilimia nne zinatolewa kwa wanawake na vijana, huku asilimia mbili zikitolewa kwa watu wenye ulemavu.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Wakati mwafaka madaktari watumie ving'ora, vimulimuli






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
kulangwasos@gmail.com.

HIVI karibuni Dar es Salaam, nilikuwa harusini na rafiki yangu Dk. Davvy, ambaye ni daktari bingwa wa magonjwa ya binadamu katika hospitali maarufu jijini humo.

Wakati tukiendelea kuserebuka, Dokta alipokea simu na ghafla akatoka nje ili kuchelea kelele ndani ya ukumbi. Akakaa kitambo kidogo na mara akarejea na kuniambia kuna jambo limejiri.

Nilishtuka na kujiuliza kulikoni? Lakini akaniambia, ni mambo ya kawaida kwao madaktari kuitwa linapotokea jambo hospitalini. Akaniambia kuna mgonjwa mahututi anahitaji huduma yake.

Nami bila ajizi nikamruhusu, kwani ndio wito alio nao duniani. Akaondoka na kigari chake IST, akajikongoja kwenda alikoitwa. Kwa alivyokuwa na utu, naamini mawazo yote aliyaelekeza katika kuokoa maisha. Hiyo ni pamoja na wito na kiapo alichoapa.

Lakini akiwa njiani, akasimamishwa na askari wa usalama barabarani, akasimama na kujieleza alikokuwa akienda. Lakini, askari akamtaka amwonyeshe leseni yake ya udereva.

Bahati mbaya wakati anabadili nguo ili aende harusini hakukumbuka kuchukua leseni, akamjibu ameisahau nyumbani. Lakini, akaishia kuambiwa aegeshe gari pembeni, naye akatii.

Wakati ameegesha pembeni, askari wale wawili wakaendelea kusimamisha magari mengine na kuhoji madereva. Dk. Devvy akagundua kuna jambo linaendelea ili kuruhusiwa.

Kwa kuwa alikuwa na shauku ya kufika hospitalini kumwona mgonjwa wake, akaona isiwe shida, akamwita mmoja wa maaskari wale...haraka akamwambia nenda.

Wakati anajiandaa kukaa sawa kwenye gari, mara yule askari akasimamisha bodaboda na kupanda, akaondoka kwa kasi kuelekea kule kule alikokuwa akienda Dokta, mwelekeo wa hospitali.

Huku nyuma Dokta akaondoka, lakini mbele akakumbana na kikwazo cha taa nyekundu. Kwa kuwa alishaumwa na nyoka, akaona atii tu mpaka ibadilike. Akawa pale mpaka ya kijani ilipowaka, akaondoka.

Moja kwa moja hospitalini akaelekea kilipo chumba cha upasuaji alimokuwa mgonjwa wake. Mlangoni akakuta kundi la watu na mmoja wao akiwa ni yule askari, wakisikiliza maelezo ya muuguzi.

Kumbe alikuwa akiwajulisha kuhusu kifo cha mgonjwa wao aliyekuwa anasubiri huduma ya Dk. Devvy. Dokta alipokaribia, macho yake yakagongana moja kwa moja na ya askari.

Yule muuguzi akamkaribisha Dk. Devvy na kumpa pole, akisema yuke mgonjwa wetu bahati mbaya Mungu kamchukua. Dokta akaonyesha kusawajika na kusikitika sana, huku akimpa pole yuke askari.

Ulikuwa wakati mgumu sana kwa askari aliyemzuia Dokta, kisha akamruhusu kwa namna anayojua yeye, kisha akapanda bodaboda kwenda kwa mgonjwa wake ambaye kumbe ni dada yake, lakini akashindwa kumhudumia na kupoteza maisha.

Bila shaka angemwacha Dokta kwa maelezo yake yale, huenda bila shaka dada mtu asingepoteza maisha siku hiyo, angalau angesogeza muda wa kuishi au angeishi maisha yake aliyopangiwa duniani.

Baada ya hapo, Dokta akarudi harusini akatukuta tukiendelea na akanisimulia mkasa wote unaoumiza, lakini hakukuwa na la kufanya, zaidi ya kusema alimwacha yule askari akiomba radhi kwa maumivu na uchungu mkubwa.

Hayo ndiyo yanayotokea leo, kwamba wapo wazito wanaopewa kipaumbele katika matumizi ya barabara hata zisizoruhusiwa magari mengine kupita, huku watu muhimu kama madaktari wakisahaulika.

Juzi hapa nikaona kwenye video mtandaoni, kiongozi si wa ngazi ya juu sana, akienda kijijini kwao kwa msafara wa magari yakitamba barabarani kumlinda.

Njiani magari yote yakiwa yamewasha taa na miongozo ya barabara mingine mingi, hata kusababisha hata mabasi ya abiria kupisha yakiegeshwa pembeni, kumoisha mheshimiwa apite! Inatafakarisha.

Huko nyuma tulizoea kuona kwa Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu, lakini leo ni wengi, madaktari hapana!

Hivi jiulize unayesoma safu hii, kuna barabara moja inaelekea huko kwingine na hospitalini penye mgonjwa mahututi, daktari anatakiwa kwenda kumwokoa mtu, nani aruhusiwe kwanza? Hekima na busara vitawale!

**Alamsiki!**

BIASHARA

# Wavuvi Mwanza walia thamani ya sangara wao imeshikwa na wanunuzi

• Watetezi waja juu, inaliwa na 'mabondo'



Muuza samaki aina ya sangara katika Soko la Kimataifa Mwaloni, jijini Mwanza, Sikitu Tizigaranyila, . **PICHA: ANTHONY GERVAS.**

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

HIVI sasa katika soko la samaki nchini, ni vigumu kuacha kumtaja sangara, maana wametapakaa kila kona kunakouzwa bidhaa hiyo.

Kimsingi, sangara ni aina ya samaki kutoka kwenye familia iitwayo 'latidae'na wanaishi katika maji baridi. Pia inatajwa, samaki hao wanapatikana kwa kiasi kidogo katika maji baridi yaliyochangamana na maji chumvi.

Asili yake sangara ni katika Mto Nile, ambako inaungana na Ziwa Victoria, ukielekeza maji kuelekea Bahari ya Mediterranean Kaskazini mwa Afrika, inakoyatiririsha.

Katika nchi za Afrika Mashariki, sangara yuko katika orodha ya samaki muhimu kiuchumi na kwa chakula. Kama ilivyo kwa samaki wengine, wana kiasi kikubwa sana cha protini, hivyo wanabaki kuwa lishe muhimu sana kwa umma unaowala.

Sangara, naye anakula nyama (carnivore), hivyo ana sifa ya kula samaki wenzake na kuchangia kupungua hifadhi ya samaki.

Kimaumbile, inatajwa sangara anao uwezo wa kukua kufika urefu wa mita mbili na uzito wa kilo 200. Hivyo, ni samaki anayeweza kukua sana.

Nchini Tanzania wanapatikana kwa wingi Ziwa Viktoria, ambako wapo baadhi ya wakulima wanaowafuga kwa kutumia vizimba.

### SIMULIZI YA MABONDO

Katika kumuandaa sangara aliyevuliwa kwenda sokoni, mara nyingi hutolewa sehemu ndani ya tumbo lake, iliyo maarufu kwa jina la mabondo.

Hayo yanayotokana na samaki sangara na yanatajwa kuwapo katika masoko ya ndani na nje, kuliko samaki wenyewe wanaouzwa viwandani.

Wadau wa uvuvi na utetezi wa haki za wavuvi wa samaki wanasema mabondo hayo pamoja na kuwa na bei kubwa, hayawanufaishi wavuvi wenyewe, badala yake wanaonufaika ni wawekezaji viwandani wanaonunua samaki na kuwasafirisha nje ya nchi.

Mkurugenzi wa Shirika la Kutetea Haki za Wavuvi (FUO) jijini Mwanza, Juvenary Matagili, anasema mabondo ni 'dili' kubwa kibiashara katika masoko ya ndani na nje, kuliko samaki wenyewe, lakini wahusika wa uvuvi bado hawanufaiki.

"Bei ya mabondo yatokanayo na samaki aina ya sangara ni kubwa maradufu katika masoko ya ndani na nje ya nchi. Kilo moja ya mabondo katika masoko ya ndani kwenye mialo ni kuanzia shilingi 150,000 hadi shilingi 800,000 kulingana na soko lenyewe," anasema.

Pia, anafafanua kilo moja ya soko ya mabondo hayo nje nchi ni kati ya Sh. milioni moja na Sh. milioni 3.5, Matagili akifafanua kwamba, wao wakiwa watetezi wa haki za wavuvi, wanaona umuhimu wa kuwasaidia, ili nao wanufaike moja kwa moja na mabondo, kuliko kwa nyama ya samaki wenyewe wanaouzwa viwandani.

Hapo ndipo mtetezi huyo wa wavuvi anaenda mbali akihoji wale samaki ambao wanaonekana hawafai kuchakatwa minofu yao viwandani, je hupelekwa wapi?

### FAIDA ZA SANGARA

Katibu Mtendaji wa shirika hilo, watetezi wa haki za wavuvi, Demai John, anataja faida za uvuvi wa sangara ni pamoja na kupata minofu, mabondo, utumbo unaotengenezwa chakula cha kuku, mifupa pamoja na mafuta ya kupikia, hata kufanya hakuna kinachotupwa kutoka kwa samaki huyo.

Pia, anataja changamoto za uvuvi wake ni kuwapo usalama mdogo wa wavuvi ziwani na kuibiana nyavu za uvuvi.

Hata hivyo, anaahidi injini za mitumbwi na vifaa vya matumizi yake, wanatarajia kutengeneza mfumo wa kisasa kuwaunganisha kwenye mtandao (GPS) ili kusaidia kuzuia wizi huo.

Pia, John anataja mikakati yao ni kuishauri Wizara ya Uvuvi na Mifugo kuweka mikakati ya kuhakikisha mabondo, yanatengenishwa moja kwa moja na samaki kabla hawajapelekwa viwandani kuuzwa.

Anasema, lengo kuu ni kufanya uwe mradi unaojitegemea kuliko kuuzwa kiholela na kusababisha serikali kupoteza mapato yatokanayo na bidhaa hiyo, kwani sekta ya uvuvi inachangia pato kubwa la taifa.

Jopn anaiomba serikali itoe ruzuku kwa wavuvi, ili wapate huduma katika maeneo yao ya kazi, kama vile afya, elimu, maji barabara k wenye visiwa wanavyofanyia shughuli zao.

### KAZI ZA FUO

Katibu Mtendaji, Demai John, anaeleza kazi zao zinajumuisha kutetea haki za wavuvi, mathalan katika mabadiliko ya bei kila wakati ya mazao ya samaki viwandani.

Anafafanua kwamba liwekuwa tatizo kubwa kwa wavuvi na wafanyabiashara wa samaki, hivyo wao shirika wanatumika kuwa daraja la kuwasaidia wavuvi kupata haki sahihi kutoka katika bidhaa zao.

John anasema, bei ya samaki inaposhuka huwa wanawasiliana na vyama vyote vyenye viwanda vya kuchakata minofu ya samaki, pamoja na Chama cha Wafanyabiashara Viwandani na Wakulima (TCCIA), ili kulipatia ufumbuzi tatizo hilo, wao shirika wanatumika kuwa daraja la kuwasaidia wavuvi kupata haki zao.

Jambo lingine analolisema, ni kuwatetea kuhusu masuala ya tozo ya leseni za uvuvi, nyavu na vyombo mbalimbali vya uvuvi kama vile mitumbwi, nyavu na sheria zinazozungumzia aina ya vifaa hivyo, ikiwemo karabai.

Vifaa vingine anavitaja kuwa ni taa za uvuvi zinazotumia nguvu ya miale ya juu, maarufu sola na mwanga wa taa za aina nyingine na viwango vyake; matundu ya nyavu za uvivu kwa kiwango kinachotakiwa na serikali, ili isiathiri mazalia ya samaki.

Katika hilo, Katibu Mtendaji huyo ana maoni kwamba serikali kuzifanyia marekebisho sheria ya zana za uvuvi ziwe zinafanana au sheria moja ya Afrika Mashariki, kuhusu ukubwa wa matundu ya nyavu zinazoruhusiwa kuvulia samaki.

John anatoa mfano wa uhalisi uliopo ni kwenye ukubwa wa matundu ya nyavu za uvuvi, akitoa mfano nchini Uganda kunaruhusiwa ukubwa wa milimita sita; Tanzania na Kenya zina milimita saba.

John anaeleza jingine, akianza kuelimisja kuwa guba ni maeneo yenye uoto wa asili uliomo kando ya ziwa au baharini yasiyokuwa na mawimbi makubwa, hivyo wavuvi wanaokiuka sheria wakikutwa wanavua humo, huchukuliwa hatua ikiwemo kunyang'anywa vifaa haramu.

Eneo la pili; anaeleza FUO inasaidia kulinda rasilimali zilizopo ndani ya maziwa na bahari, ikielimisha kuepukana na uvuvi haramu na kutotumia zana zinazochangia uchafuzi wa mazingira.

Vilevile, John anawahamasisha wavuvi wasitumie zana mbadala za uvuvi ambazi zimepigwa marufuku ama ziwani au baharini, ikiwamo ukataji miti ovyo, hata ukasababaisha uharibifu wa mazingira.

### WANAVYOIANGALIA JAMII

John anaeleza, pia wanaielimisha jamii suala zima la kuachana na vitendo vya ukatili wa kijinsia, hasa kwa wanawake na watoto wanaopeleka huduma za biashara na vyakula, pia elimu ya ya afya.

Aidha, anafafania kuwa wanaelimisha jamii ya wavuvi kujikinga na maambukizi ya virusi vya Ukimwi, wakishirikiana na madaktari wa jiji na wataalamu wa afya kutoka shirika la kimataifa la AMREF. '



# Mtaka: Wenye fistula wasijifiche nyumbani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amewataka wanawake wanaosumbuliwa na ugonjwa wa fistula kuacha kujificha majumbani kwa kuona aibu na badala yake waende kwenye vituo vya kutoa huduma za afya ili kupata matibabu.

Mtaka alitoa rai hiyo jana alipokuwa akizindua kambi ya utoaji wa matibabu ya fistula katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma.

"Nitoe rai kwa wanawake wote wanaosumbuliwa na magonjwa ya fistula waache kujificha kwa kuona aibu badala yake waende kupatiwa matibabu kwakuwa huduma hiyo inapatikana hapa kwenye hospitali yetu ya rufani mkoa wa Dodoma, kuendelea kujificha kuendelea kujisababishia matatizo mengine makubwa zaidi, hivyo mjitokeze kupata matibabu," alisema Mtaka.

Mtaka alipongeza hatua na jitihada zinazofanywa na wadau wa fistula nchini na kuahidi kuwapa ushirikiano katika kutimiza dhamira yao ya kupunguza fistula nchini mpaka itakapofika mwaka 2030.

"Nichukue nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru wadau wote wa fistula kwasababu huu ugonjwa umekuwa ni kati ya magonjwa yenye changamoto hapa nchini hivyo nawashukuru sana kwa hili na nitawaunga mkono," alisema.

Kwa upande wake, Daktari Bingwa wa Magonjwa ya kinamama na upasuaji wa fistula ambaye ni Rais wa Chama cha Madaktari wa Fistula Tanzania, Dk. James Chapa, aliahidi kushirikiana na madaktari bingwa wenzake ili kuhakikisha wanapunguza kiwango cha kuenea kwa ugonjwa wa fistula nchini kufikia mwaka 2030.

# Maombi ya ajira za afya na elimu yafikia 158,186

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imesema hadi sasa maombi ya ajira yaliyopekelewa kikamilifu kupitia mfumo kwa kada ya Afya na Elimu ni 158,186.

Hali hiyo inaonyesha mwitikio mkubwa wa maombi ya ajira huku kibali cha ajira za watumishi hao kilichotolewa kwa kada za mbalimbali za afya ni 7,612 huku walimu ni 9,800.

Hata hivyo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Innocent Bashungwa, ameongeza siku nne kwa waombaji ambao wameshindwa kukamilisha maombi yao.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Ofisi hiyo, Nteghenjwa Hosseah, awali waombaji walitakiwa kutuma maombi yao kuanzia Aprili 20, mwaka huu na mwisho ulikuwa juzi lakini kwasasa mwisho wa kutuma ni Mei 8, mwaka huu.

"Kuhusu idadi ya waombaji wa ajira hizo mpaka kufikia tarehe 03.05.2022 saa 5:59 usiku waombaji waliokamilisha maombi yao kupitia mfumo kwa Kada ya Afya ni 39,053 na Kada ya Elimu ni 119,133 hivyo jumla ya waombaji wote ni 158,186,"alisema.

Alisema Waziri Bashungwa ameongeza siku hizo ili wale wote walioshindwa kukamilisha maombi yao.

"Wale walioshindwa kukamilisha maombi kwasababu zozote zile watumie muda huu wa nyongeza kukamilisha maombi yao kupitia kiunganishi cha ajira.tamisemi.go.tz " alisema.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akizungumza na Balozi Humphrey Polepole, anayekwenda kuiwakilisha Tanzania nchini Malawi, ofisini kwake, jijini Dodoma jana. **PICHA: OMR**

# Kutupa taka barabarani faini 300,000/-

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAKAZI wa Jiji la Dodoma wameonywa kuacha kutupa taka kwenye miundombinu ya barabara na atakayebainika atatozwa faini ya Sh.300,000.

Mkuu wa Idara ya Mazingira na Udhibiti wa taka ngumu wa Jiji hilo, Dickson Kimaro, alitoa onyo hilo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufanya ukaguzi wa miti ya maua iliyowekwa barabarani kwenye mitaa mbalimbali.

Kimaro alisema kwenye ziara yake amebaini vyungu vya maua vilivyoko barabarani, baadhi vimewekewa taka huku vingine vikiharibiwa kwa kugongwa.

"Lengo la vyungu hivi vya miti ya maua ni kupendezesha Jiji lakini cha kusikitisha baadhi ya watu wakiwamo madereva wa vyombo vya moto hawajali miundombinu hiyo kwa kuwa wanahihujumu kwa kuigonga na mitungi mingine imegeuzwa kuwa sehemu ya kutupia takataka," alisema.

Hata hivyo, alisema kutokana na hali hiyo Jiji litaendelea kutoa elimu zaidi kwa wakazi ili kuwa na tabia ya kuipenda, kuitunza na kuilinda miundombinu ambayo inayowekwa barabarani.

Alisisitiza Jiji litaendelea kutoa adhabu zake zilizowekwa kwa wale wote watakaobainika kuhujumu miundombinu.

"Adhabu hizo ni pamoja na watakaobainika kuharibu miundombinu ikiwamo vyungu hivyo vya maua atapigwa faini Sh. 300,000 au kununua visivyopungua vitatu," alisisitiza.

Aliwakumbusha wakazi wa Dodoma ambao miundombinu hiyo ipo karibu na maeneo yao ya makazi na ofisi kuwa mabalozi wa kulinda na kuisimamia ili isiharibiwe na kuimwagilia maji.

"Hapa naomba niwaombe wakazi na wadau wa Jiji la Dodoma pamoja na kuilinda kwa wale ambao wapo karibu na miti hiyo waimwangilie na kuilinda," alisema.

Awali akizindua upandaji wa maua mwishoni mwa wiki, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, aliwataka wadau wa mazingira wa Jiji ambao majengo ya ofisi zao yapo barabarani kuimwangilia, kuilinda na kuitunza ili isinyauke.

Shekimweri alisema kuwa miti hiyo ya maua iliyopandwa kwenye vyungu vinatakiwa kusimamiwa, kulindwa na kumwangilia maji kwa uaminifu mkubwa ili kuwa na mazingira ya kuvutia ya Jiji hilo.





## Rungwe yavuka lengo ukusanyaji wa mapato

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

HALMASHAURI ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya imekusanya Sh. bilioni 1.3 sawa na asilimia 104 katika kipindi cha robo tatu ya mwaka 2021/22.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Mpoki Mwankuga, aliiambia Nipashe jana kuwa makusanyo hayo ni kuanzia Januari hadi Machi, mwaka huu, na kwamba makisio yalikuwa ni chini ya kiasi hicho.

Pia alisema kuanzia Julai, mwaka jana, hadi Machi, mwaka huu, walikusanya Sh. bilioni nne sawa na asilimia 77 ya makisio ya mwaka ambayo yalikuwa Sh. bilioni tano.

'Mapato haya yametokana na vyanzo kama ushuru wa mazao, ada ya ushuru, ada ya leseni, mapato kutokana na mali za halmashauri, ushuru wa maliasili, mapato ya hisa na ada za shule na Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii Iliyoboreshwa (ICHF)," alisema Mwankuga.

Makusanyo ya fedha hizo, alisema yalitumika kwenye ujenzi wa miradi ya kutolea huduma za afya kama vile ujenzi wa Kituo cha Afya Kinyala, miundombinu ya elimu na huduma zingine za kijamii.

Alisema katika mapato hayo, ada za shule zilikusanywa kwa asilimia 91, ushuru wa maliasili ukiwa asilimia 86, mazao asilimia 80 na mapato mengine yakiwa asilimia 159.

"Nalipongeza Baraza la Madiwani pamoja na watumishi wa halmashauri kwa usimamizi mzuri wa rasilimali ambazo zimesaidia kukusanya kiasi hiki cha fedha. Nina imani kwamba fedha hizi zitatumika kuboresha miundombinu ya afya, barabara, shule kilimo na maeneo mengine ya kutolea huduma za kijamii," alisema Mwankuga.

Alisema kipindi cha mwaka 2021/22, halmashauri ilipata hati safi ya ukaguzi wa hesabu baada ya kuwapo kwa ushirikiano mzuri baina ya chama, serikali, wataalamu na Baraza la Madiwani.

Baadhi ya madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe walisema miongoni mwa matarajio ni kuona wakiendelea kukusanya fedha nyingi ili kuboresha miundombinu ya barabara ambazo ni korofi kipindi cha msimu wa mvua.

Walisema barabara kutoka Ushirika hadi Masukulu imekuwa korofi katika msimu wa mvua baada ya kutopitika kutokana na kujaa maji na utelezi.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi ya mchepuo wa Kiingereza ya Mkapa, jijini Mbeya, wakinawa mikono kwa kutumia vifaa maalumu jana, kwa ajili ya kujikinga na maradhi mbalimbali ya kuambukiza kama vile kuhara na UVIKO - 19. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wakulima mahindi walia uhaba wa mbolea

**Na Grace Mwakalinga,** MBOZI

WAKULIMA wa mahindi katika Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, wamesema pamoja na kutumia mbegu bora za mahindi na zenye tija kutokana na kipato chake kuwa kikubwa, bado wanakabiliwa na kikwazo cha upatikanaji wa mbolea.

Kutokana na kupanda kwa gharama za pembejeo za kilimo hususani mbolea, kumesababisha wakulima kutopata mavuno mengi kulinganisha na ilivyokuwa awali kabla ya kupanda kwa zana hizo.

Mmoja wa wakulima wa zao hilo, Ibrahim Sikanyika, alisema hali ya mavuno msimu huu hairidhishi kwa sababu wameshindwa kumudu gharama za mbolea na kwamba hadi sasa mbolea ya kukuzia na kupandia inauzwa kati ya Sh. 100,000 na 120,000 kwa mfuko wa kilo 50. Sikanyika alisema gharama hiyo ni kubwa kulinganisha na ilivyokuwa msimu uliopita walipokuwa wakinunua kwa kati ya Sh. 65,000 na 75,000.

"Gharama za maisha zimepanda. Kila kitu bei juu, kwa kweli tunaumia sana. Tunashindwa hata kutimiza malengo yetu maana hata pembejeo za kilimo bei imepaa. Msimu huu wengi wetu tumelima mazao yetu kwa kutumia mbolea za samadi na mashamba mengine kutowekewa mbolea kabisa," alisema Sikanyika.

Naye Frank Mkondya alisema pamoja na msimu wa mvua kuchelewa kuanza katika ukanda wa Nyanda za Juu Kusini, mbegu za mahindi aina ya 'panner' na 'pioneer' zimefanya vizuri, lakini upatikanaji wa mbegu hizo maeneo mengi ni shida.

Mkondya alisema mbegu za 'Panner' zimesaidia kupunguza makali kwa wakulima kwa sababu wamepata mavuno ya kuridhisha na kwamba wangevuna mengi endapo bei ya mbolea ingekuwa nafuu.

Ofisa Kilimo wa Kijiji cha Anseketwa, Kata ya Ihanda, alisema pamoja na vikwazo wanavyokabiliana navyo wakulima, jambo la muhimu ni kuzingatia kanuni bora za kilimo ili kupata mavuno mengi.

Alisema maofisa ugani wamekuwa wakiwatembelea wakulima kuwapa elimu ya kilimo bora na mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ili kupata mavuno mengi shambani.

Meneja wa Kampuni ya Corteva Agri Science, ambayo inazalisha na kusambaza mbegu za Panner na Pioneer, Tolio Mafie, alisema mahitaji ya mbegu hizo ni makubwa lakini kampuni itajitahidi kuongeza uzalishaji.

Mafie alifafanua kuwa ikiwa mkulima atazingatia ushauri wa wataalamu, anaweza kuvuna magunia 35 hadi 40 kwa ekari moja, hivyo aliwashauri kuachana na kilimo cha mazoea na kujikita zaidi katika kilimo biashara.

# Wananchi kicheko ujio mradi wa maji

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

ZAIDI ya wakazi 2,000 wa Kata ya Itamboleo na maeneo jirani yanayozunguka eneo hilo, wanatarajiwa kunufaika na mradi mkubwa wa maji baada ya serikali kutoa Sh. milioni 631 kwa ajili ya kukamilisha mradi huo.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Reuben Mfune, alisema juzi kuwa fedha hizo zilitolewa na serikali kutokana na mkopo wa masharti nafuu kwa ajili ya mapambano dhidi ya UVIKO- 19 ili kutatua tatizo la huduma hiyo katika kata ya Itamboleo.

"Rais wetu mpendwa Samia Suluhu Hassan ametuletea Sh. milioni 631 kwa ajili ya kukamilisha mradi wa maji unaojengwa katika kata ya Itamboleo. Kutokana na mradi huo, zitapatikana fursa mbalimbali ikawamo ajira kwa wanakijiji," alisema Mfune.

Meneja wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Mbarali, Mhandisi Samuel Hechei, alisema mradi huo unatekelezwa kwa awamu mbili. Alisema awamu ya kwanza itakuwa ujenzi wa banio, tangi la lita 300,000, vituo vinane vya kuchotea maji na ujenzi wa mtandao wa bomba kilomita 15.9.

Kwa mujibu wa meneja huyo, awamu ya pili itahusu utekelezaji katika vijiji vya Matebete, Mbalino na Kapunga na itahusisha ujenzi wa mtandao wa bomba kilomita 72.2, tangi la lita 200,000 na ujenzi wa vituo 19 vya kuchotea maji na utagharimu Sh. milioni 3.9.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Mbarali, Hashimu Mwalyawa, alimpongeza Mkuu wa Wilaya kwa kutekeleza vizuri ilani ya uchaguzi ya chama hicho ikiwamo mradi huo ambao alisema utamaliza tatizo la maji katika kata hiyo na kuwapa wananchi nafasi ya kuzalisha mali.

Aliwaomba wananchi kutoa ushirikiano wa hali na mali katika kutekeleza ujenzi wa mradi huo na kuwasihi kuepukana na vitendo vya wizi wa vifaa hivyo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali ambaye ni Diwani wa Itamboleo, Twalibu Lubandamo, alisema eneo hilo lilikuwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa maji na kwamba mradi huo utasaidia kumtua mama ndoo kichwani.

Alisema mkataba wa utekelezaji wa mradi ulitiwa saini Januari 10, mwaka huu, na unatarajiwa kutekelezwa ndani ya miezi sita na utakapokamilika utakuwa na uwezo wa kuhudumia wananchi 22,543.



# Serikali yaunda wakala uwezeshaji wananchi kiuchumi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, amesema serikali imeunda wakala wa uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa ajili ya kufuatilia na kuhakikisha fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya wananchi kwa lengo la kupiga hatua ya maendeleo. Soraga alisema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, wakati akijibu swali la mwakilishi wa viti maalumu wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Bihindi Hamad Khamis, aliyetaka kujua mchakato wa utoaji wa fedha za wajasiriamali.

Alisema fedha za wajasiriamali zimewekewa utaratibu ambao kwanza vikundi vinatakiwa kujisajili kwa ajili ya kupata fedha hizo, kuratibiwa na kufahamika na sheha. Alisema hicho ni miongoni mwa kigezo muhimu kwa sababu hizo ni fedha za serikali ambazo zimelengwa kwa wajasiriamali wadogo na baadaye zinatakiwa zirudishwe kwa ajili ya kufaidika watu wengine.

"Mheshimiwa Spika fedha za Covid-19 zimelengwa kwa wajasiriamali wadogo kwa lengo la kuona wanajiimarisha kibiashara ambapo baadaye zinatakiwa zirudishwe na kuwafikia watu wengine," alisema.

Akifafanua, Soraga alisema Serikali ya Zanzibar imetenga fedha kwa makundi mbalimbali ya wajasiriamali ikiwamo wakulima wa mazao ya baharini ambayo ni mwani na majongoo ya baharini.

"Mheshimiwa spika huu ni wakati muafaka kwa wajasiriamali wetu kujitokeza kuchangamkia fedha za uwekezaji katika sekta mbalimbali ili kujiinua kiuchumi na uwekezaji," alisema.




Waziri wa Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Sada Mkuya, akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Zaidi ya walimu 800 wa sayansi kuajiriwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali, imesema inakusudia kuajiri walimu wa masomo ya sayansi 816 kwa lengo la kukabiliana na uhaba wa walimu wa aina hiyo ili kusaidia ufaulu wa masomo hayo katika shule za Unguja na Pemba.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Abdulgulam Hussein, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Mtambwe, Habib Ali Mohamed, aliyetaka kujua mikakati ya wizara katika kuajiri walimu wa masomo hayo.

Alikiri wizara kukabiliwa na tatizo la uhaba wa walimu kwa masomo ya sayansi ikiwamo Baiolojia, Kemia, Hesabati na Fizikia na kusababisha ufaulu usioridhisha kwa wanafunzi.

Alisema mahitaji ya walimu wa Fizikia kwa shule zote za Unguja na Pemba ni 259, walimu 74 wa somo la Kemia na upande wa somo la Hisabati ni walimu 430 wakati 53 wanahitajika katika somo la Baiolojia.

Alisema walimu hao wataajiriwa kwa mujibu wa mwongozo wa serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.

"Mheshimiwa Spika napenda kuwajulisha Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ipo katika mchakato wa nafasi za ajira kwa watumishi wapya wa Wizara ya Elimu na pia kipaumbele tumeweka kwa walimu wa masomo ya sayansi," alisema.

# Uhaba wa madaktari Unguja, Pemba wapata ufumbuzi

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuimarisha utoaji wa huduma bora za afya, Serikali ya Zanzibar imesema ipo katika mchakato wa kuajiri wafanyakazi 4,000 ikiwamo madaktari katika hospitali za Unguja na Pemba.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Afya, Hassan Khamis Hafidh, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Tumbatu, Haji Omar Kheir, aliyetaka kujua lini wizara itaanza kuajiri wafanyakazi wa hospitali ikiwamo madaktari ili kukabiliana na uhaba uliopo sasa.

Alisema kufuatia ujenzi wa hospitali 10 za wilaya ya Unguja na Pemba zinazoendelea sasa, wizara imepanga kuajiri madaktari wapya 3,000.

Alisema mchakato wa kuajiri umeanza na miongoni mwa vipaumbele vilivyowekwa ni pamoja na kuzipatia madaktari hospitali za vijijini.

"Mheshimiwa Spika napenda kulijulisha Baraza la Wawakilishi kwamba tumeanza mchakato wa kuajiri madaktari wapya 3,000 kwa ajili ya hospitali 10 zinazojengwa katika Wilaya za Unguja na Pemba kwa ajili ya kukabiliana na tatizo hilo," alisema.

Alisema miongoni mwa vipaumbele vya ajira kwa madaktari ni pamoja na hospitali zilizopo katika visiwa vidogo vya Unguja na Pemba ili kukabiliana na changamoto za sekta ya afya. Alisema hospitali hizo zitapatiwa madaktari pamoja na wafanyakazi watakaotoa huduma za kujifungua kwa wajawazito na watoto.

"Nimhakikishie Mwakilishi wa Jimbo la Tumbatu katika kisiwa kidogo hicho kwamba tumepanga kuajiri madaktari na wasaidizi wake katika visiwa vidogo zinapatikana ili kukabiliana na changamoto hizo," alisema.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetenga jumla ya Sh. bilioni 36 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali 10 za wilaya ikiwamo moja ya mkoa inayojengwa hapo mjini Lumumba ambayo itakuwa na sifa ya hospitali ya mkoa yenye ghorofa nne.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**Ndugu ABDI KHAMIS ABDALL** Anatangaza kupotelewa na Cheti cha kidato cha Nne, Certificate, Diploma na Degree. Kidato cha Nne Index **no S.3910.0071/2010** kilichotolewa na baraza la Mitihani katika shule Shule ya Secondary Mitiulaya iliyopo Wilaya ya Wete Pemba Mwaka 2010. Cheti cha Certificate kilichotolewa na chuo cha Zanzibar Institute of Financial Administration kilichopo Chwaka Zanzibar Mwaka 2012 Reg No. 11/CFA4/199. Cheti cha Diploma kilichotolewa na chuo cha Zanzibar Institute of Financial Administration kilichopo Chwaka Zanzibar Mwaka **2014 Reg No. 12/OFA5/134.** Cheti cha Degree kilichotolewa na chuo cha Insititute of Finance Management (IFM) kilichopo Dar es salaam Mwaka 2018 Reg No. IMC/BAC/15/90049 Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Taarifa ya Polisi: DOD/DOD/RB/157812/2022**

## NAFASI ZA KAZI

Kampuni ya Madawa iliopo Dar es salaam inahitaji **MEDICAL REPRESENTATIVE.**

Kwa mawasiliano piga simu namba **0713 786300.**

## KUPOTEA KWA PASSPORT YA KUSAFIRIA




**Ally Twalib Ally**

Anatangaza kupotelewa na Passport ya kusafiria yenye namba **Ab167338**

Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa katika kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Ally Twalib Ally kwa simu namba **0621-959800**

POLISI TAARIFA: **DSM/PHQ/RB/173915/2022**

## KUPOTEA KWA VYETI



Ndugu **DAVID KINDANDA** Anatangaza kupotelewa na Cheti cha kidato cha Nne, Cheti cha kidato cha sita na cheti cha Diploma in Education. Cheti cha Kidato cha Nne Index namba **S.0462/0037** kilichotolewa na baraza la Mitihani katika shule Shule ya Sekondari WIGEHE Mwaka 1998. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0346-0517** kilichotolewa kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia shule ya sekondari UYUI mwaka 2001 na Cheti cha Diploma in Education chenye index namba **E515-0034** kilichotolewa na CHUO CHA UALIMU KASULU mwaka 2004. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Taarifa ya Polisi:**KAS/KAS/RB/020/2022**

## KUPOTEA KWA VYETI



Ndugu **DAVID KINDANDA** Anatangaza kupotelewa na Cheti cha SHAHADA YA UALIMU na **ACADEMIC TRANSCRIPT** yenye usajili namba **2006010170** vilivyotolewa na CHUO KIKUU CHA ARUSHA mwaka 2010. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi:**KAS/KAS/RB/020/2022**

## MNADA WA HADHARA MARUDIO

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD, Dalali tajwa hapo chini** tutauza kwa mnada wa hadhara dhamana za mdaiwa Sugu Ismail Abdallah Magari kama ilivyotangazwa kwenye gazeti;-

| Mdaiwa/ mdhamini | Dalali | Aina ya Dhamana | Tarehe ya mnada - Mahali |
|---|---|---|---|
| Ismail Abdallah Magari | MMAuctioneers And Debt Collections And Co.Ltd | Toyota Coaster T.628 DRU | 20./05/2022 Mwanza Yard |
| Ismail Abdallah Magari | MMAuctioneers And Debt Collections And Co.Ltd | Toyota Coaster T.915 BXN | 20/05/2022 Mwanza Yard |

**Masharti ya Mnada**

Minada yote itafanyika mahali dhamana zilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**MAWASILIANO PIGA: 0718 730242 / 0677001063**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa Amri ya Mahakama ya Mwanzo ya Chamwino Mjini ya tarehe 07/02/2022 Madai na 164/2022 tutauza Nyumba noja Plot no. 9 Block "BBB" Chang'ombe Extension Jijini Dodoma mali ya Hussein Juma ili kufidia deni analodaiwa na Farouk Mohamed. Mnada utafanyika nyumba ilipo na itauzwa kama ilivyo siku tarehe 20/05/2022 saa nne asubuhi (04:00).

Pia idhini ya mteja wetu KIMWAGA AUTO WORKS CO. LTD, tutauza kwa mnada wa hadhara (kochi, Makabati, Tv, Radio, Vitanda, Magodoro, na Friji) mali ya Crepin bulamu kufidia deni analodaiwa. Mnada wa utafanyika katika uwanja wa mpira uliopo Nzuguni C mbuyuni siku ya tarehe 08/05/2022 saa nne asubuhi (04:00).

**WASILIANA NASI ILI UONESHWE MALI YA CHAGUO LAKO KABLA YA SIKU YA MNADA KWA NAMBA 0715 170 553**

**MWAMBA AUCTION MART AND RECOVERIES**
**P.O.BOX 429 DODOMA – TANZANIA**
**OFFICE LOCATION:**
**CCM REGIONAL BUILDING ROOM No. 9**
**0715170553 / 0756011439**

## TENDER NOTICE

Ubalozi wa kifalme wa Saudi Arabia unatangaza tenda ya kampuni ya Ulinzi inayoweza kufanya kazi nao, kila kampuni inayoomba ilete barua ya maombi ubalozini.

Mwisho wa tenda ni wiki mbili kuanzia tangazo la gazeti hili.

**Kwa mawasiliano piga namba**
**+255222667833 / +255222668203**
**Ada Estate Plot No. 44 Galu Street**
**Email: tzemb@mofa.gov.sa**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mhakama ya mwanzo ya wilaya ya Temeke**
**Kituo cha Jumuishi Mkoa Dar es salaam**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 783/ 2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU JUMANNE MWINSHEHE MTEMU KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MWANAHAMISI MWINYIMADI MASANGA**

**TANGAZO**

(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/ maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 6 Mwezi wa 6 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

**Imetolewa leo tarehe 22 Mwezi wa 04 Mwaka 2022.**



## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ZAINAB H. MGUDE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Toyota station wagon yenye usajili namba T 536 ANK . kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: KW/RB/2067/2022**

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0782253676

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Marekani yadaiwa kuisaidia ujasusi Ukraine

**WASHINGTON,** MAREKANI

MAREKANI imedaiwa kuvipatia vikosi vya Ukraine taarifa za kijasusi ambazo zimesaidia kuwalenga na kuwauwa majenerali wa Russia nchini humo.

Kwa mujibu wa ripoti kutoka gazeti la New York Times, ambalo liliwanukuu maofisa wa ngazi ya juu wa nchi hiyo, taarifa hizo zilihusu shughuli za vikosi vya Russia na mahala vilipo na vinavyo hama hama.

Taarifa hizo pia zilitumiwa na vikosi vya Ukraine wakati wa mashambulio ambayo yalipelekea kuuawa kwa maofisa wa kijeshi wa Russia.

Maofisa wa Ukraine wanadai Majenerali 12 wa ngazi ya juu waliuawa katika mzozo huo, huku ikidhaniwa kuwa morali ya chini miongoni mwa wanajeshi wa Russia imewalazimisha maofisa wa ngazi ya juu jeshini kwenda karibu zaidi na maeneo ya mapigano.

Hawakubainisha ni mangapi kati ya mashambulio haya walisaidiwa na ujasusi wa Marekani.

Msemaji wa Ikulu ya White House, alikosoa taarifa ya gazeti la New York Times, akisema kichwa chake cha habari kilikuwa kinapotosha na kutowajibika.

Msemaji wa Baraza la Usalama la Taifa, Adrienne Watson aliongeza kuwa Marekani huipatia Ukraine ujasusi unaohusu uwanja wa mapambano ili kulinda nchi yao na bila lengo la kuwauwa Majenerali wa Russia

Russia yadaiwa kuingia ndani ya kiwanda cha chuma cha Azovstal

Kwa mara ya kwanza, vikosi vya Russia vimeweza kuingia ndani ya kiwanda cha Azovstal huko Mariupol na kuna uwezekano kinatekeleza mashambulizi yake katika eneo hilo.

Kulingana na tathmini ya Taasisi ya Utafiti wa Vita (ISW), kufanikiwa kuingia ndani ya kiwanda hicho inatokana na kutumia siku kadhaa za mapigano makali kwenye eneo la kiwanda hicho, ambapo wapiganaji wa mwisho wa Ukraine katika mji huo wanadhibiti.

Taasisi hiyo yenye makao yake makuu nchini Marekani pia ilisema ulinzi wa Ukraine kwa kiasi kikubwa umezuia hatua zilizopigwa na Russia mashariki mwa Ukraine.

Vikosi vya Ukraine hadi sasa vimezuia vikosi vya Russia kuunganisha mashambulizi yao kusini mashariki mwa Izyum na magharibi mwa eneo la mapambano mjini Donetsk-Luhansk.

Magharibi mwa Ukraine, majaribio ya Russia ya kuvuruga usafirishaji wa misaada kwenda Ukraine kutoka nchi za Magharibi na kupunguza kasi ya juhudi za ugavi wa silaha pia imeonekana kutofanikiwa, ilisema ISW.

Vikosi vya Russia vilizidisha mashambulizi ya anga dhidi ya miundombinu ya usafiri karibu na vituo vya reli huko Lviv na Transcarpathia siku ya Alhamisi, lakini hatimaye vilishindwa kusababisha madhara makubwa.

BBC haijaweza kuthibitisha ripoti kuhusu mashambulizi ya wanajeshi wa Russia katika kiwanda hicho.

Katika kanda fupi ya video iliyochapishwa katika mtandao wa Telegram, kamanda wa Azov Denis Prokopenko alisema ananajivunia kuongoza wanajeshi ambao wanafanya juhudi kubwa kudhibti shinikizo la adui.

Rais Volodymir Zelensky, aliwasilisha ombi kwa Umoja wa Mataifa kuokoa maisha ya watu waliojificha ndani ya kiwanda hicho.

'Kila mtu ni muhimu kwetu. Tunaomba usaidizi wenu ili kuwaokoa'," Zelensky alimwambia katibu mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres



Moshi ukifuka kutoka ndani ya kiwanda cha chuma cha Azovstal nchini Ukraine baada ya vikosi vya Russia kufanikiwa kuingia ndani. **PICHA: BBC**

# Mchungaji akamatwa akidai kuujua mlango wa mbinguni

**ABUJA, Nigeria**

MCHUNGAJI mmoja nchini Nigeria, Ade Abraham anashikiliwa na polisi baada ya kuwatoza watu pesa ili kuwaonyesha lango linaloelekea mbinguni.

Mchungaji huyo alieleza mlango huo uko eneo la kusini -magharibi mwa nchi hiyo na anaweza kuwaonyesha kwa malipo maalum.

Mchungaji Abraham alikamatwa baada ya mmmoja wa wafuasi wake, ambaye alisema alimtoza naira 310,000 sawa na dola 750; £600 kulitazama eneo linakopatikana katika mji wa Araromi-Ugbeshi, uliopo katika jimbo la Ekiti.

Kiongozi huyo wa kidini alikiri kwamba alikuwa ametoa kauli kuhusu mlango huo wa mbinguni, akisema kuwa ni Mungu anayemtumikia ambaye alimfunulia ili kuijaribu imani ya watu wa kanisa lake, lakini hakujapokea malipo yoyote.

Jumuiya ya Wakristo wa Nigeria imetoa taarifa ya kumkana kiongozi huo, wakati polisi wa jimbo la Ekiti wanaendelea kukusanya taarifa kutoka kwa wafuasi wa kanisa lake na kuanzisha uchunguzi.

Kanisa la Mchungaji Abraham awali lilikuwa katika jimbo la Kogi na baadaye likahamia katika jimbo la Kaduna , kabla ya kuhamia kusini na wafuasi wake katika kambi aliyoijenga katika jimbo la Ekiti.

## Msumbiji yapanga kudhibiti utitiri wa Makanisa

**MAPUTO,** MSUMBIJI

MSUMBIJI inapanga kuanzisha sheria mpya ambayo itadhibiti shughuli za makanisa ikiwamo kulipisha kodi kila mwaka.

Waziri wa masuala ya Haki, Katiba na Dini nchini humo, Helena Kida alisema kuwa tathmini ya serikali imefichua kuna dalili mbaya wakati kuna ongezeko la idadi ya makanisa yanayosambaa kila mahali.

Msumbiji ina jumla ya madhehebu 900 rasmi yaliyosajiliwa, lakini mengi ya hayo yanayoendesha shughuli zake kiholela.

Baraza la Wakristo wa Msumbiji linaunga mkono vipengele vingi vya sheria iliyopendekezwa, likisema linatambua kuwa serikali inataka kuleta utaratibu mzuri wa usajili wa nyumba za ibada.

Kipengele cha kuyatoza kodi makanisa hata hivyo kinayatia hofu makanisa hayo.

"Ni suala ambalo lilizungumziwa, lakini hatukufikia muafaka," alisema Rais wa CCM Felicidade Chirindza

## Mwanamke mbaroni kuwasaidia Al-Shabaab

**WASHINGTON,** MAREKANI

MWANAMKE mmoja wa Kisomalia mwenye uraia wa Uholanzi, amefunguliwa mashtaka ya kuchangisha pesa kwa ajili ya kusaidia kundi la ugaidi la al-Shabaab.

Kulingana na shirika la upelelezi la Marekani (FBI),Farhiya Hassan ( 38), alionekana na hatia ya kutoa usaidizi kwa kikundi cha al-Shabaab.

Mwendesha mashitaka mkuu wa jimbo la Eastern Virginia Jessica Aber,nyaraka na ushahidi unaonyesha kuwa kikundi cha watu watatu akiwemo Farhiya, kimekuwa kikikusanya fedha kwa muda wa miaka mitatu kutoka katika nchi kadhaa kwa ajili ya kuisaidia kundi hilo la kigaidi.

Farhiya anasemakana kuwa kila mara alikuwa akichukua pesa hizo na kuituma moja kwa moja kwa kikundi cha al-Shabaab.

Miongoni mwa nchi alizochangisha pesa ni pamoja na Uholanzi, ambako aliwambia watu kuwa anachangisha pesa kwa sababu za kibinadamu.

HABARI MICHEZO

# NAHIMANA AREJESHWA NCHINI HARAKA KUINUSURU NAMUNGO

**Na Saada Akida**

KISA nafasi nne za timu zitakazoiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa msimu ujao, uongozi wa Namungo FC, umemrejesha kikosini kipa chaguo la kwanza, Jonathan Nahimana ili kuisaidia timu hiyo kufikisha malengo yake.

Nahimana hajasimama langoni katika mechi mbili zilizopita za timu hiyo ambapo ilianza kufungwa na Yanga na ikalazimisha sare na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba.

Namungo FC iko katika nafasi ya tatu ikiwa na pointi 30, Azam FC nafasi ya nne kwa alama 29 sawa na Kagera Sugar inayoshika nafasi ya tano, Mbeya City iko nafasi ya sita ikijikusanyia pointi 28 sawa na Geita Gold FC iliyoko katika nafasi ya saba.

Taarifa za uhakika zilizoifikia gazeti hili kutoka ndani ya Namungo FC, zinasema Nahimana ambaye aliondoka nchini na kuelekea kwao Burundi baada ya kutokuwa na sintofahamu kati yake na viongozi wa timu hiyo, mipango inafanyika kumrejesha kikosini.

**Chanzo chetu kinadau Mrundi huyo aliamua kurudi kwao baada ya kutofahamu hatima ya fedha zake za us ajili anazodai.**

Mtoa habari huyo alisema viongozi wa Namungo wanahitaji kuona kikosi chao kinakuwa imara ili kupata matokeo chanya katika mechi zilizobakia za ligi.

"Kuna vita kubwa sana katika kugombea nafasi nne za juu hasa ukizingatia kuna timu nne, ikiwamo sisi Namungo FC tunahitaji kumaliza ligi msimu huu katika nafasi hiyo, hatuwezi kufikia malengo bila ya kuweka sawa timu yetu," kilisema chanzo chetu.

Mwenyekiti wa Namungo FC, Hassan Zidadu, alisema hakuna tatizo lolote na mchezaji huyo na alienda kwao Burundi kwa ajili ya matatizo ya kifamilia.

"Hakuna ukweli wowote kuhusu kipa huyo, hayuko nchini si kwa sababu ya haelewani na viongozi bali aliienda kwao kwa ajili ya matatizo yake binafsi, atarejea nchini na kuendelea na majukumu yake ya kazi baada ya pia taratibu zake za vibali vya kuishi vitakapofanyiwa kazi," alisema Zidadu.

Nipashe lilimtafuta Nahimana ambaye alisema yuko kwao Burundi lakini anafanya mazoezi binafsi.

"Sasa mambo yako vizuri na pia suala lingine lililokwamisha ni VISA iliisha muda wake, likikamilika hilo nitarejea kikosini kuendelea na majukumu yangu katika klabu yangu katika vita vya kumaliza nafasi tatu," alisema Nahimana.




Moja ya timu zinazoshiriki Ligi ya Betika Sodo Bingwa iliyoko katika Kituo cha Lindi. Ligi hiyo imeanzishwa kwa ajili ya kuibua vipaji vipya vya soka mikoani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Ligi ya Betika Sodo safi*

**Mwandishi Wetu**

VITA ya kuwania ubingwa wa Ligi ya Soka ya Mchangani (Betika Sodo Bingwa Ligi) imeshika kasi ikiwa imebaki michezo mitatu ili kufikia tamati.

Ligi hiyo inayodhaminiwa na Kampuni ya Michezo ya Kubashiri ya Betika inafanyika katika vituo vya Mwanza, Ruvuma, Lindi, Kilimanjaro, Iringa na Dar es Salaam.

Katika kituo cha Dar es Salaam kesho Jumamosi na Jumapili kwenye uwanja wa Msisiri, Kinondoni timu nane zitashuka uwanjani kusaka pointi tatu muhimu.

Espanyola itakuwa dimbani kesho kusaka pointi tatu na kujiimarisha kileleni itakapocheza dhidi ya Smart Fighter saa 11 jioni wakati mapema Jaga watawavaa Morocco Square.

Jumapili Care Boys itacheza dhidi ya Hard Number mchezo utakaoanza saa 10:30 jioni, ikiwa na kumbukumbu nzuri ya ushindi kwenye mchezo uliopita baada ya kuichapa Morocco Square bao 1-0.

Hard Number yenyewe imetoka kupata ushindi mnono katika mechi iliyopita ilipoichapa Smart Fighter mabao 3-0 yaliyofungwa na Saidi Habibu, Yusuph Shomari na Salumu Mohamed.

Mechi ya mapema Jumapili itakuwa ni kati ya Mapanga dhidi ya Swazi Inter, mchezo utakaoanza saa 9:00 Alasiri.

Meneja Masoko wa Betika, Nelson Mwanuzi alisema wanadhamini ligi hiyo tangu imeanza kwa malengo ya kuibua vipaji vya soka la mchangani.

"Mashindano katika mikoa yote yanafanyika kwenye viwanja vya mtaani na moja ya kanuni ni timu kucheza kwa kutumia mpira wa makaratasi 'chandimu' bila njumu," alisema Mwanuzi.

Aliongeza Betika inafarijika kuwa sehemu ya kuibua vipaji hivyo kwenye Ligi ya Sodo wanayoidhamini.

# Insta United yapata neema

**Na Saada Akida**

KAMPUNI ya Utengenezaji na Uuzaji wa Magari ya GF Trucks imeingia mkataba na Klabu ya Insta United kuelekea msimu mpya wa mashindano ya Kombe la Ndondo (Twende Pamoja).

Mgeni rasmi katika hafla ya kusaini mkataba, Naibu Mstahiki Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Said Khimji alisema anaamini Insta United itafanya vizuri na kuibuka na ubingwa wa msimu huu katika michuano hiyo kutokana na mipango yake na udhamini walioupata.

Khimji alisema GF Trucks ni wadau wa soka wa muda mrefu kwa sababu waliwahi pia kudhamini timu ya Mbao FC, Alliance zote za Mwanza na sasa DTB FC inayoshiriki Ligi ya Championship.

"Ninaimani udhamini huu utaleta ushindani na kufanya timu ya Insta kufanya vizuri na hatimaye kutwaa ubingwa wa Ndondo Cup," alisema Khimji.

Naye Mtendaji Mkuu wa Insta United, Chiku Said alisema lengo la kuanzisha timu hiyo ni kuinua na kuendeleza vipaji vya vijana.

Mkurugenzi wa GF Trucks, Ally Karmali alisema kwa muunganiko huo utakuwa na faida kwa pande zote kutokana na timu hiyo kufanya vizuri katika mitandao ya kijamii ikiwamo Instagram ambapo ndipo anaamini watatangazika zaidi.

# Daraja la Kwanza Zanzibar yarejea

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Chuoni inatarajia kuvaana na Gulioni katika mechi ya Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Amaan, visiwani hapa.

Ligi hiyo imerejea tena kuanzia leo baada ya kusimama ili kupisha mwezi wa Ramadhani uliomalizika mapema wiki hii.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya Kundemba dhidi ya Bridge Star.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Zanzibar, Hashim Salum, alisema maandalizi yote kuelekea michezo hiyo ya Ligi Daraja Kwanza Kanda na ile ya Ligi Kuu Zanzibar yamekamilika.

Salum alisema licha ya Bodi ya Ligi kufanya maandalizi katika kiwango kizuri ili ligi hiyo imalizike kwa wakati, bado changamoto ya uwanja hususani viwanja vya Mau imekuwa ikiwakwamisha.

"Tunaendelea kuhakikisha kalenda yetu inakwenda sawa sawa na ligi inamaliza kwa wakati ili kupata timu mbili zitakazopanda daraja licha ya kuwapo na changamoto ya viwanja," alisema Salum.

Kundemba yenye pointi 39 ndio vinara wa ligi hiyo ikifuatiwa na Dulla Boys yenye alama 38 huku nafasi ya tatu ikikaliwa na Chuoni yenye pointi 36.

## ZISIKUPITE

### RAPHINA ANUKIA BARCA

BARCELONA wameongeza juhudi za kumsajili winga wa Timu ya Taifa ya Brazil, Raphinha mwenye umri wa miaka 25. (***Telegraph***)

### PALACE KUMUUZA ZAHA

WINGA wa Crystal Palace na Ivory Coast, Wilfried Zaha mwenye umri wa miaka 29, huenda asisaini mkataba mpya na klabu hiyo na akauzwa msimu huu wa joto kwani mkataba wake unakamilika mwaka 2023. (***Times***)

### TRAORE, BARCA ZAJIPANGA

BARCELONA hawana nia ya kulipa ada ya euro milioni 30 kubadilisha uhamisho wa mkopo wa winga wa Hispania, Adama Traore mwenye umri wa miaka 27 kutoka Wolves na kuwa na mkataba wa kudumu badala yake wanataka mpango wa kubadilishana wachezaji. (***Fabrizio Romano***)

### MARTINEZ ATAJWA ARSENAL

KLABU ya Arsenal inataka kumsajili mshambuliaji wa Inter Milan na Timu ya Taifa ya Argentina, Lautaro Martinez, ingawa wakala wa kiungo huyo mwenye umri wa miaka 24 amesema mchezaji mwenyewe "hajafikiria" kuondoka klabu yake ya sasa. (***Goa**l*)

### GINTER AIKATAA VILLA

MLINZI wa kati wa Borussia Monchengladbach na Ujerumani, Matthias Ginter mwenye umri wa miaka 28 amekataa uhamisho wa msimu wa joto kwenda Aston Villa na badala yake atajiunga na Freiburg. (***Football Insider***)

### SARR AKARIBIA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle imepewa ofa ya kumsajili mshambuliaji wa Watford na Timu ya Taifa ya Senegal, Ismaila Sarr mwenye umri wa miaka 24 kwa pauni milioni 40. (***Football Transfers***)

### RAMSAY KUTUA LIVERPOOL

LIVERPOOL wanamfuatilia mchezaji wa Aberdeen na Timu ya Taifa ya Scotland, Calvin Ramsay mwenye umri wa miaka 18. (***Liverpool Echo***)

### BRIGHTON YAMFUATA HAMER

KLABU ya Brighton inamtaka beki wa Coventry City, Gustavo Hamer mwenye umri wa miaka 24. (***Football Insider***)

### HLOZEK MAMBO BADO

KLABU ya West Ham huenda ikamkosa mshambuliaji wa Sparta Prague na Jamhuri ya Czech, Adam Hlozek mwenye umri wa miaka 19 licha ya kupewa nafasi ya kumsajili kwa mkopo msimu huu wa joto. (***90min***)


### SPURS, LEEDS VITANI

KLABU za Tottenham Hotspur, Leeds United na Fulham zinamtaka winga wa zamani wa Derby na Timu ya Taifa ya England, Malcolm Ebiowei mwenye umri wa miaka 18. (***Sun***)

### FULHAM YAANZA KUJIPANGA

KLABU ya Fulham iliyopanda daraja imeweka mikakati ya kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Sweden, Viktor Gyokeres mwenye umri wa miaka 23 kutoka Coventry City. (***Football Insider***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA: CITY TUNAHITAJI MUDA

## Ili kurejea mchezoni baada ya kuondolewa na Madrid iliyokuwa...

**MADRID,** Hispania

PEP Guardiola amesema wachezaji wake wa Manchester City watahitaji "muda" kushughulikia kile kilichotokea dakika za mwisho dhidi ya Real Madrid baada ya kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, hapo juzi.

City waliongoza kwa bao 1-0 wakiwa na jumla ya ushindi wa 5-3 huku sare iliingia dakika ya 90 kwa Real Madrid kufunga mabao mawili ndani ya dakika moja na kusawazisha.

Karim Benzema alifunga kwa penalti katika kipindi cha kwanza cha muda wa ziada na kuipa nafasi ya kutinga fainali ambayo itakutana na Liverpool mjini Paris Mei 28, mwaka huu.

**Guardiola alikiri baada ya mchezo huo kuwa Real Madrid walikuwa kwenye kiwango cha ajabu.**

"Wana huzuni," alisema Guardiola.

"Walikaribia kufika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Lakini sasa tunahitaji muda kushughulikia hilo na kurejea kwenye michezo minne iliyobaki katika Ligi Kuu."

"Wakijaribu kupambana kwa hali na mali, lakini mambo yalikuwa magumu sana kwetu."

"Hatukuwa wazuri vya kutosha lakini hatukuteseka sana. Baada ya kufunga tulikuwa bora, tulipata nafasi yetu.

"Hatukuteseka sana lakini hatukucheza kwa uwezo wetu wote, ni kawaida katika nusu fainali.

"Tulikuwa karibu, lakini soka haitabiriki. Wakati mwingine inakuwa hivi na lazima ukubali."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,224

MECHI KALI
GENOA
VERSUS
JUVENTUS
1 | 3.91
X | 3.34
2 | 1.91

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# JEZI YA MARADONA YAUZWA BEI KUFURU

**LONDON,** England

JEZI ambayo mchezaji wa Argentina, Diego Maradona aliyovaa alipofunga bao la "Mkono wa Mungu" dhidi ya England katika fainali za Kombe la Dunia mwaka 1986 imeuzwa kwa bei iliyoweka rekodi ya dunia ya dola milioni 9.28 kwenye mnada wa Sotheby jijini London.

Bei hiyo inazidi rekodi ya hapo awali ya jezi iliyovaliwa katika mechi, ambayo ilikuwa dola milioni milioni 5.64 zilizolipwa mwaka 2019 kwenye jezi ya Babe Ruth wa New York Yankees aliyecheza mwaka 1928 hadi 1930.

Maradona alivaa jezi hiyo katika robo fainali dhidi ya England mwaka 1986 ambapo alifunga mabao yote mawili ya Argentina katika ushindi wao wa 2-1.

Bao la kwanza lilikuwa maarufu la "Mkono wa Mungu" ambapo alipiga mpira kwa kipa wa England, Peter Shilton.

Maradona, aliyefariki Novemba, 2020 alisema lengo lilikuwa "kidogo kutoka kwa kichwa cha Maradona, na kidogo kwa mkono wa Mungu."

Bao lake la pili linazingatiwa na wengi kuwa moja ya mabao bora zaidi kupamba Kombe la Dunia.

Maradona aliwapiga chenga wachezaji nane wa England na kumfunga Shilton na kuwapa Argentina uongozi wa mabao 2-0. Baadaye liliitwa bao la karne na FIFA.



# Barca kutotumia Camp Nou




**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona imethibitisha kufanyia marekebisho ya Uwanja wa Camp Nou na wametangaza kuwa timu hiyo msimu wa 2023-24 itatumia Uwanja wa Olympic kwenye eneo la Montjuic ndani ya jiji hilo.

Uboreshaji utaanza Juni, baada ya kumalizika kwa msimu huu, baada ya bodi kuthibitisha kiasi cha euro bilioni 1.5 ili kuweza kufanya maboresho ya uwanja huo maarufu duniani.

Inatarajiwa kuwa maboresho yatachukua miaka minne kwa kazi zote kumalizika, hii inamaanisha kuwa Barcelona watapaswa kuhama kwa msimu uja na kuhamia kwenye uwanja w Olympic ambao unatumika n timu ya Espanyol.

Klabu ya Barcelona itawe kuutumia uwanja wa Camp Nu kwa msimu unaofuata, baad ya msimu 2023-24, huku wal tarajiwa kupunguza idadi watazamaji kwa asilimia 50 kv sababu ya ujenzi.

"Kitakuwa kiwanja bora d niani, ndani ya jiji bora dunian ndani ya nchi bora dunian alisema rais wa Barcelona, Jo Laporta

Kiwanja kipya kitakuwa umbo la mstatili, huku juu ku wa kumefunikwa.

## HABARI MICHEZO

# DK. TULIA MGENI RASMI MBEYA TULIA MARATHONI

**MWANDISHI WETU,** Mbeya

SPIKA wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Ackson, anatarajia kuwaongoza wanariadha mbalimbali katika ufunguzi wa mbio za Mbeya Tulia Marathoni (MTM) zitakazofanyika leo kwenye Uwanja wa Sokoine jijini hapo.

Zaidi ya wanariadha 2,000 wanatarajiwa kushiriki katika mbio hizo zenye lengo la kukusanya fedha kwa ajili ya kusaidia miundo mbinu ya afya na elimu.

Wanariadha hao watachuana katika umbali wa mita 100, 200, 400, 800 na 1500 ambapo mabingwa wapya wa msimu wa tano watapatikana.

Kesho mtanange utahamia katika mbio ndefu za barabarani ambazo pia zitaongozwa na Dk. Tulia, bosi wa Taasisi ya Tulia Trust inayoratibu mbio hizo kila mwaka.

**Meneja wa Tulia Trust, Jackline Boaz alisema maandalizi ya mbio hizo yako katika hatua za mwisho na leo pazia la us ajili kwa mbio za baraba rani linafungwa.**

"Wale wa mbio ndefu watajisajili hadi Ijumaa, tunafarijika kuona mwamko wa wakimbiaji msimu huu umekuwa mara mbili ya msimu uliopita," alisema Boaz.

Aliongeza mshindi wa kwanza hadi watatu katika mbio za uwanja za mita 100, 200, 400, 800 na 1500 kila mmoja ataondoka na medali na fedha taslimu.

"Jumamosi ndiyo itakuwa kilele cha mbio hizi, ambapo mchuano utahamia kwenye mbio za kilomita 10, 21 na 42," Boaz alisema.

Kocha wa Timu ya Taifa ya Riadha, Suleiman Nyambui, alisema hiyo ni moja ya mbio tatu ambazo wanariadha wake watajipima kabla ya kuelekea Uingereza katika Michezo ya Madola.

Timu hiyo tayari iko jijini hapa tangu juzi na leo wanariadha wake wanne wa mbio fupi watachuana kusaka ubingwa wa MTM huku wale wa mbio ndefu wakitarajiwa kuchuana kesho.



Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Ackson (wa pili kushoto), akiongoza baadhi ya wabunge kufanya mazoezi ya kujiandaa na mbio za Mbeya Tulia Marathon zitakazofanyika leo kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini Mbeya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shy-Rose ajipanga kuibeba CHANETA

**Na Saada Akida**

MAKAMU Mwenyekiti mpya wa Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA), Shy-Rose Bhanji amesema wataandaa mipango kabambe kurejesha hadhi ya mchezo huo nchini hasa katika ushindani katika ngazi ya kimataifa.

Shy-Rose ameibuka mshindi katika nafasi hiyo kwa kupata kura 34 kwenye uchaguzi mdogo huku mpinzani wake, Juliana Manyerere hakuambulia kura hata moja.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Shy-Rose alisema atashirikiana vyema na viongozi wenzake kuhakikisha wanashiriki mashindano ya kimataifa yakiwamo ya Afrika Mashariki na Kati, Afrika na Kombe la Dunia.

"Tumerejea katika mchezo tunaoufahamu na kazi yetu ni kupanga mipango itakayowavutia wadau, tutashirikiana katika kurudisha hadhi na heshima ya mchezo huu kama awali," alisema Shy-Rose.

Aliongeza mikakati mingine waliyonayo ni kutafuta wadhamini watakaousaidia kuinua mchezo huo.

Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CHANETA ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Netiboli Mkoa wa Singida, Farida Juma, alisema matumaini yao mchezo huo utarudi katika mfumo mzuri.

Nafasi ya Katibu Mkuu katika uchaguzi huo ilikwenda kwa Rose Mkisi aliyepata kura 19 kwa kuwashinda wapinzani wake watatu ambao ni, Jacqueline Sikozi, aliyepata kura nane, Rahma Kilimba aliyepata kura saba huku Damiani Chonya hakupata kura hata moja.


4,601,040

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 07/05/22 | 17:00 | Burnley vs Aston Villa | 2.87 | 3.17 | 2.41 |
| 02. 07/05/22 | 17:00 | Brentford vs Southampton | 2.21 | 3.37 | 3.02 |
| 03. 07/05/22 | 19:00 | Sassuolo vs Udinese | 2.25 | 3.56 | 2.82 |
| 04. 07/05/22 | 19:30 | Brighton vs Manchester Utd | 2.62 | 3.21 | 2.58 |
| 05. 07/05/22 | 19:30 | Hertha BSC vs Mainz | 2.52 | 3.31 | 2.62 |
| 06. 07/05/22 | 20:00 | Benfica vs Porto | 2.74 | 3.43 | 2.39 |
| 07. 08/05/22 | 16:00 | Leicester vs Everton | 2.31 | 3.22 | 2.97 |
| 08. 08/05/22 | 16:00 | Venezia vs Bologna | 2.93 | 3.27 | 2.31 |
| 09. 08/05/22 | 17:15 | Villarreal vs Sevilla FC | 2.30 | 3.25 | 3.05 |
| 10. 08/05/22 | 17:45 | Feyenoord vs PSV Eindhoven | 2.41 | 3.62 | 2.58 |
| 11. 08/05/22 | 19:00 | Salernitana vs Cagliari | 2.35 | 3.26 | 2.87 |
| 12. 08/05/22 | 19:30 | Espanyol vs Osasuna | 2.59 | 3.14 | 2.74 |
| 13. 08/05/22 | 22:00 | Atletico Madrid vs Real Madrid | 2.37 | 3.30 | 2.90 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 06/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 5359 | Mathare United vs Sofapaka | 5.60 | 3.35 | 1.69 |
| 15:15 | 5263 | Sarawak vs Negeri Sembilan | 2.50 | 3.20 | 2.75 |
| 16:00 | 4347 | Kedah vs Melaka | 1.65 | 3.69 | 4.47 |
| 16:30 | 1815 | Navbahor Namangan vs Bunyodkor | 2.84 | 2.89 | 2.49 |
| 16:30 | 2867 | Surkhon Termez vs Kokand 1912 | 3.50 | 2.82 | 2.18 |
| 16:30 | 3377 | Metallurg Bekabad vs Qizilqum | 2.65 | 2.70 | 3.05 |
| 17:00 | 5655 | Jazira Abu Dhabi vs Ajman Club | 1.53 | 4.10 | 4.89 |
| 17:30 | 1370 | Gaz Metan Medias vs Clinceni | 4.06 | 3.71 | 1.77 |
| 17:30 | 3589 | Mohammedan SC vs Churchill Brothers | 2.07 | 3.45 | 3.06 |
| 18:00 | 2452 | Sigma Olomouc vs Mlada Boleslav | 2.43 | 3.39 | 2.83 |
| 18:00 | 3239 | Kryliya Sovetov vs Dinamo Moscow | 3.17 | 3.32 | 2.16 |
| 19:00 | 2463 | Radomiak Radom vs Zaglebie Lubin | 2.24 | 3.16 | 2.96 |
| 19:15 | 1337 | Crotone vs Parma | 2.59 | 3.34 | 2.54 |
| 19:30 | 1222 | Ismaily SC vs Al Masry Club | 2.03 | 2.98 | 4.07 |
| 19:30 | 1679 | Horsens vs Lyngby | 2.15 | 3.20 | 3.10 |
| 19:30 | 2290 | Paderborn vs Sandhausen | 1.86 | 3.76 | 3.61 |
| 19:45 | 1512 | AL Wahda Scc (UAE) vs Al Sharjah SC | 2.02 | 3.57 | 3.08 |
| 19:45 | 3675 | Inter vs Empoli | 1.13 | 8.09 | 14.80 |
| 20:00 | 1369 | Silkeborg vs Randers | 1.71 | 3.88 | 4.28 |
| 20:00 | 4394 | Gaziantep BB vs Kayserispor | 1.83 | 3.73 | 3.83 |
| 20:00 | 5672 | Hatayspor vs Trabzonspor | 2.45 | 3.48 | 2.64 |
| 20:30 | 1419 | Botosani vs Dinamo Bucuresti | 1.61 | 3.76 | 5.15 |
| 20:30 | 4234 | SuperSport Utd vs Moroka Swallows FC | 2.22 | 2.80 | 3.80 |
| 21:00 | 1404 | Cambuur vs Waalwick | 2.18 | 3.43 | 3.03 |
| 21:15 | 5009 | Luka Koper vs Tabor Sezana | 1.53 | 3.90 | 5.26 |
| 21:30 | 1360 | Lecce vs Pordenone | 1.19 | 6.15 | 12.90 |
| 21:30 | 1591 | Como vs Cremonese | 4.96 | 3.91 | 1.61 |
| 21:30 | 1760 | Cosenza vs Cittadella | 1.81 | 3.42 | 4.27 |
| 21:30 | 2279 | Alessandria vs Vicenza | 2.22 | 3.23 | 3.13 |
| 21:30 | 2960 | Frosinone vs Pisa | 2.00 | 3.36 | 3.56 |
| 21:30 | 3575 | Perugia vs Monza | 3.42 | 3.37 | 2.04 |
| 21:30 | 4188 | Benevento vs Spal | 1.62 | 3.81 | 4.95 |
| 21:30 | 4680 | Legia Warszawa vs Gornik Zabrze | 1.91 | 3.36 | 3.60 |
| 21:30 | 4866 | Brescia vs Reggina | 1.44 | 4.27 | 6.56 |
| 21:30 | 5253 | VfL Bochum vs Arminia Bielefeld | 2.13 | 3.43 | 3.13 |
| 21:30 | 5833 | Ascoli vs Ternana | 1.76 | 3.61 | 4.25 |
| 21:45 | 1033 | Drogheda Utd vs St Patricks | 4.57 | 3.50 | 1.68 |
| 21:45 | 1643 | UCD Dublin vs Dundalk FC | 6.81 | 4.47 | 1.37 |
| 21:45 | 3812 | Sunderland vs Sheffield Wed | 2.62 | 3.22 | 2.58 |
| 21:45 | 3972 | Shelbourne vs Sligo Rovers | 2.97 | 2.87 | 2.41 |
| 21:45 | 4216 | Inverness vs Partick Thisle | 2.20 | 3.12 | 3.32 |
| 21:45 | 5452 | Charleroi vs Racing Genk | 3.08 | 3.48 | 2.16 |
| 21:45 | 5619 | Derry City vs Bohemians FC | 1.73 | 3.41 | 4.39 |
| 22:00 | 1541 | Shamrock Rovers vs Finn Harps | 1.24 | 5.03 | 10.65 |
| 22:00 | 2095 | Las Palmas UD vs Mirandes | 1.63 | 3.96 | 4.65 |
| 22:00 | 3636 | Smouha Club vs Pyramids | 3.78 | 3.13 | 2.04 |
| 22:00 | 4398 | Genoa vs Juventus | 3.91 | 3.34 | 1.91 |
| 22:00 | 5612 | Levante vs Real Sociedad | 2.95 | 3.41 | 2.28 |
| 22:00 | 5709 | Lille vs Monaco | 3.74 | 3.59 | 1.89 |
| 22:15 | 5773 | Boavista vs Vitoria Guimaraes | 3.03 | 3.28 | 2.27 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Nipashe Ijumaa Mei 6, 2022



Shy-Rose ajipanga kuibeba CHANETA UK. 23




Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohammed Mchengelwa, akipiga penalti kwa ajili ya uzinduzi rasmi ziara ya Kombe la Dunia Tanzania. Uzinduzi huo umeshuhudiwa na Mkurugenzi Mkuu wa Coca Cola Kwanza, Unguu Sulay na Rais wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF), Wallace Karia (mwenye sharti jeupe). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Coca cola yalileta tena Kombe la Dunia nchini

**Na Mwandishi Wetu**

MCHEZAJI wa Timu ya Soka ya Taifa ya Ufaransa, David Trezeguet, anatarajiwa kutua na Kombe la Dunia nchini ifikapo Mei 31, mwaka huu, ikiwa ni kwa mara ya nne mfululizo Tanzania imefanikiwa kulipokea kombe hilo kati ya nchi tisa za Afrika.

Akizungumza jana katika uzinduzi wa ziara hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa Coca cola nchini, Unguu Sulay, alisema kwa mara nyingine Tanzania imefanikiwa kupata tiketi ya kulishuhudia kombe hilo kabla ya kuelekea nchini Qatar katika fainali za mwaka huu.

Sulay alisema ziara hiyo ni mwendelezo wa kampuni yao kurudisha kiu na mipango ya Tanzania katika kusaka tiketi ya kushiriki kwa mara ya kwanza fainali hizo katika miaka ya baadaye.

"Sio kila Taifa linapata hii nafasi, Tanzania imekuwa ni tofauti tumepata nafasi hii kwa mara ya nne kulipokea kombe hili halisi na watu kupata nafasi ya kupiga nalo picha," alisema Sulay.

Naye mgeni rasmi katika uzinduzi huo Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mohammed Mchengerwa, robo tatu ya Watanzania wanapenda michezo na ziara hii inakuja kuwapa fursa watu wengi wenye rika tofauti kushuhudia kombe hili ambalo Tanzania inafanikisha ndoto za kuandaa fainali hizi.

"Serikali na wizara yetu ya michezo imefarijika na ziara hii ikiwezeshwa na ninyi Coca cola, Rais wetu (Samia Suluhu Hassan) anapenda michezo na tuna ndoto za siku moja tuje kuandaa fainali hizi ingawa kwanza tunatakiwa kuamini inawezekana na baada ya hapo tujenge miundombinu kama vile viwanja," alisema Mchengerwa.

Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia alisema ziara hii ya kombe hili ni mwendelezo wa ushirikiano bora kati ya kampuni hiyo na TFF katika maendeleo ya mpira.

"Coca cola imekuwa na mkono mzuri katika kuendeleza soka, sijui kama watu wanafahamu timu yetu ya Taifa Stars ya sasa ina wachezaji wengi ambao walizalishwa na mkakati wa kuzalisha vijana uliodhaminiwa na kampuni hii na ukaleta matunda bora kwa taifa letu," alisema Karia.

# Simba, Yanga zataja mwelekeo

## ●●● Ni kuelekea lala salama katika msimu huu wa 2021/22 ambao sasa...

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya Simba kukiri ina nafasi finyu ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu na kuelekeza nguvu zake zote katika mashindano ya Kombe la FA, watani zao Yanga wamelalamika kukosa bahati walipoikabili Ruvu Shooting mkoani Kigoma hapo juzi.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, aliliambia gazeti hili baada ya sare ya mabao 2-2 dhidi ya Namungo FC nafasi yao kwenye mbio za ubingwa imekuwa ngumu, lakini kama timu kubwa ni lazima ihakikishe inashinda mechi zote zilizobaki kwa ajili ya kuweka heshima ya klabu, wanachama na mashabiki wao.

"Tulikuwa na malengo matatu msimu huu, kuchukua Kombe la Mapinduzi ambalo tunalo, ubingwa wa Ligi Kuu ambapo ngoma ni ngumu kweli kweli na ni lazima kila shabiki akaelewa hivyo, lakini kwenye Kombe la FA bado kweupe, atakayekuwa kwenye ubora mechi tatu za mwisho atakuwa bingwa. Bado kwenye Ligi Kuu hatujainua ramsi mikono, lakini nguvu kubwa kwa sasa tumeiweka kwenye Kombe la FA ambapo kuna nafasi zaidi," alisema Ahmed.

**Meneja huyo alisema tayari wachezaji wa timu hiyo wameingia kambini jana kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ruvu Shooting itakayochezwa keshokutwa.**

"Kikubwa ni lazima tu tuhakikishe tunashinda mechi zetu za Ligi Kuu kama timu kubwa, Simba hata akicheza mechi ya kirafiki lazima ipate ushindi, sembuse Ligi Kuu? Isiposhinda inaumiza mioyo ya wanachama na mashabiki wa timu, isifike mahala tukakosa ubingwa, halafu ukaumiza mioyo ya watu," Ahmed alisema.

Naye Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, alisema timu yake haikuwa na bahati katika mechi dhidi ya Ruvu Shooting ambayo ilichezwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika.

Kaze alisema Yanga haikuwa na bahati katika mechi hiyo kwa sababu walipata nafasi mbili za kufunga mabao, lakini mara zote mpira uligonga nguzo.

"Kila mechi ina mfumo tofauti, tuliingia na kucheza kwenye uwanja ulioruhusu kucheza soka la pasi, ndiyo maana kipindi cha pili tukabadilika, tulibadili mfumo, ila hatukuwa na bahati kwa sababu tulipiga mwamba mara mbili, kwa maana hiyo tunarudi tena katika uwanja wa mazoezi kurekebisha makosa yaliyojitokeza. Kuhusu ubingwa bado tuna nafasi, safari ya ubingwa ipo, ila inabidi tufanye kila njia ili mechi ijayo tupate ushindi," alisema Kaze.

Hata hivyo Kocha Mkuu wa Ruvu Shooting, Charles Mkwasa, alisema katika mechi hiyo amefanikiwa kwa asilimia hamsini, lakini akalalamikia bao lao kukataliwa.

"Tumefanikiwa kwa asilimia hamsini, lakini mimi sioni tatizo ya goli tulilofunga, labda kitaalamu inaweza, maana nilikuwa mbali, naona kama lilikuwa halali. Lakini niseme tu kuwa tunasheshimu uamuzi wa mwamuzi, tunashuwakuru vijana walijitahidi, wenzetu kipindi cha pili walibadilika na kucheza mipira mirefu ya juu, vijana wangu wakawa imara kuwadhibiti. Hatukuwapa nafasi ya kukaa na mpira walipata nafasi ya kufikiri, ndiyo maana ilibidi mpaka wachezeshaji wao kina, Saido Ntibazonkiza wawatoe," alisema Mkwasa.

Alitamba waliahidi wamekwenda Kigoma kuvunja mwiko na hicho ndio kilichofanikiwa kwa kugawana pointi na vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tuliwaambia watu tunakwenda Kigoma kuvunja mwiko, tunakwenda kuwafunga. Kama si maamuzi ya mwamuzi tungefanya hivyo. Tumeumizwa, hiki ndio kinaleta shida kwenye maendeleo ya soka la Tanzania. Mpira wetu ukichezwa kwa haki, kila mtu apate anachostahili, soka lingekuwa mbali sana," alisema Masau Bwire, Msemaji wa Ruvu Shooting.

Sare hiyo imeifanya Yanga kufikisha pointi 56, wakati Ruvu Shooting wao sasa wana pointi 22 na katika msimamo wa ligi hiyo yenye timu 16 wako kwenye nafasi ya 14.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >